**MAFAHIM YA HIZB UT-TAHRIR**
**Toleo la kwanza: 1373 Hijri/1953**
**Toleo la sita: 1421 Hijri/2001**

## Mafahim ya Hizb ut-Tahrir.

Tangu katikati mwa karne ya kumi na mbili hijriya (karne kumi na nane miladiya) na ulimwengu wa Kiislamu una poromoka kutoka ambacho ni laiki yake mporomoko ulio wa haraka, na ukazorota uzorotevu unaofedhehesha. Pamoja na majaribio mbali mbali yaliojaribu kuiamsha au kuzuia kuendelea kuzorota. Haikufaulu hata jaribio moja miongoni mwa majaribio hayo. Na ukabakia ulimwengu wa Kiislamu ukitokota katika mojo wa fujo na kuzorota, mpaka sasa unahisi maumivu haya ya kubakia nyuma na mchafuko.

Amma sababu ya kuzorota kwake, hurudia kwa jambo moja nayo ni udhaifu mkubwa uliosibu fahamu katika kufahamu Uislamu. Na sababu ya udhaifu huu ni kutenganishwa nishati ya lugha ya Kiarabu na nishati ya Kiislamu pindi ulipopuuzwa mambo ya lugha ya kiarabu katika kufahamu Uislamu na kuutekeleza tangu mwanzo wa karne ya saba hijriya. Ikiwa haikutaunganishwa nishati ya kiarabu na nishati ya Kiislamu kwa kufanya lugha ya kiarabu—ambayo ni lugha ya Uislamu—sehemu muhimu isio tenganishwa nayo, utabakia uzorotevu ukiwazorotesha Waislamu kwa sababu nishati ya lugha ndio iliobeba nishati ya Kiislamu na kuungana nayo kiasi ambacho haimkiniki kuutekeleza Uislamu utekelezaji ulio kamilika bila kwayo. Na kwa sababu kupuuzwa kwake itafanya ijtihadi katika Sheria ikosekane, wala haimkiniki ijtihadi katika Sheria ila kwa lugha ya kiarabu kwa sababu lugha ya kiarabu ni sharti ya ki-msingi ndani yake. Na ijtihadi ni dharura kwa Ummah kwa sababu Ummah haisongi mbele ila kwa kuwepo ijtihadi.

Amma sababu ya kushindwa kwa majaribio yaliyojaribu kuwainusha Waislamu kupitia Uislamu, huregea kwa mambo matatu. La kwanza yake ni kukosekana fahamu funuzi juu ya fikra ya Kiislamu kwa upande wa wanaosimamia mwambo. La

pili yake ni kukosekana uwazi kamili wa twarika ya Kiislamu kwao katika kuitekeleza fikra yake. La tatu yake ni kutounganisha kwao fikra ya Kiislamu kwa twarika ya Kiislamu muungano barabara usioweza kutenganishwa.

Amma fikra, imesibiwa na mambo yaliyo ichafua, hali iliyo wafunga macho na usafi wake wengi wa Waislamu. Na sababu za uchafu huu ulianza tangu mwanzo mwa karne ya pili hijriya mpaka kuja kwa ubepari. Zilikuwa falsafa za kigeni kama ya kihindi, kifursi, na kiyunani na athari kwa baadhi ya Waislamu iliowabeba kujaribu kuleta muwafaka baina y Uislamu na falsafa hizi, pamoja na kuweko mgongano kamili baina yake na Uislamu. Ilifika majaribio haya ya muwafaka kwa taawili na tafsiri ambazo ziliweka mbali baadhi ya hakika za Kiislamu katika fahamu. Hivyo hivyo ilidhoofisha kudiriki kwao kwa Uislamu. Pamoja na haya, ilikuwa kuingia kwa baadhi ya mahasidi wa Uislamu katika boma lake—kwa unafiki—na athari katika kutia katika Uislamu ufahamu ambayo si wake bali ni zenye kugongana nayo. Hili lilipelekea katika kuufahamu Uislamu ufahamu uliochaganyikiwa kwa Waislamu wengi. Kisha ikaongezeka juu ya hayo katika karne ya saba hijriya, kupuzwa lugya ya kiarabu katika kuubeba Uislamu. Yakawa yote hayo ni sababu ya kuzorota Waislamu, Na ikazidishwa juu yake katika mwishoni mwa karne ya kumi na moja hijriya (kumi na saba miladiya) mpaka leo vita vya ki-thaqafa na ki-mishenari kisha vita vya kisiasa kutoka kwa umagharibi. Ikawa balaa juu ya balaa, na tatizo jipya juu ya matatizo yaliyotangulia. Ikawa kwa yote hayo athari ya kihakika katika kutia kosa katika sura ya Waislamu juu ya fikra ya Kiislamu mpaka ikapotea usafi wa kihakika katika ufahamu.

Amma twarika ya Kiislamu, hakika wao walikosa sura ya uwazi wake kwa daraja. Hilo baada ya kujua kuwa kuwepo kwao katika maisha ni kwa ajili ya Uislamu, na kuwa kazi ya Mwislamu maishani ni kubeba ulinganizi wa Kiislamu na kazi ya serikali ya Kiislamu ni kutabikisha Uislamu na kutekeleza hukmu zake ki-ndani na kubeba ulinganizi kwake nje na njia ya

hilo ni jihadi inayo tekelezwa na serikali. Twasema Waislamu, baada ya kujua hayo, walibadilika na wakaona kuwa kazi ya Mwislamu mwanzo ni kuchuma dunia, kisha pili waadhi na kuongoza (kwa Uislamu) dhurufu zikiruhusu. Na ikawa serikali haioni upungufu au uzito wowote katika kulegea kwake katika kutekeleza hukmu za Kiislamu wala haikuona kosa lolote katika kutopigana kwake jihadi katika njia ya Allah na kueneza Uislamu. Kisha Waislamu baada ya kuikosa serikali Yao—juu ya yale ndani yake ya unyonge na upungufu—wakaona Uislamu utarudi kwa kujenga miskiti, kutunga vitabu na malezi ya kiakhlazi wakinyamazia ubwana wa ukafiri, na ukoloni wake, juu yao.

Huu ni katika upande wa fikra na twarika. Amma katika upande wa kuzifungamanisha, wamekuwa Waislamu wakiziona hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na utatuzi wa matatizo maana yake zinazoambatana na fikra wala hawakushughulishwa nafsi zao na hukmu ambazo hubainisha jinsi ya kutatua maana yake zile ambazo hubainisha twarika. Wamejishughulisha na hukmu zilizotenganishwa na njia ya kutekelezwa kwake, na wamejishughulisha na kusoma hukmu za swala, saumu, ndoa na talaqa na wakapuuza kusoma hukmu za jihadi, ngawira (*ghanaim*), hukmu za Khilafa, ukadhi, hukmu za kharaji na zinazoshabihiana nazo. Kwa hilo wakatenganisha fikra na twarika mpaka ikazaliwa kutokamana na hayo kutowezekana kutekeleza fikra bila twarika.

Na ikaongezwa juu ya hayo yote katika mwishoni mwa karne ya kumi na tatu hijriya (kumi na tatu miladiya) kosa katika kufahamu Sheria ya Kiislamu ili kuitabikisha juu ya mujtama. Ukawa Uislamu unafasiriwa tafsiri isio kubaliana na dalili (*nusus*) zake ili iwafikiane na mujtama uliopo, lakini la wajibu ni kuubadilisha mujtama ili uwafikiane na Uislamu sio kujaribu kufasiri Uislamu ili uwafikiane na mujtama. Kwa sababu swala hapa ni kuwa kuna mujtama uliofisidika unaotakikanwa kurekebishwa na mfumo basi ni wajibu utabikishwe mfumo kama ulivyo na kubadilisha mujtama kwa jumla mbadiliko wa

ki-mapinduzi juu ya msingi wa mfumo huu. Maana yake ni lazima kwa wanaojaribu kurekebisha kwamba watabikishe Uislamu kama ulivyo kuja bila kuuangalia mujtama au zamani au wakati au mahali. Lakini wao hawakufanya hivyo bali walifanya taawili ya hukmu za Kiislamu ili iwafikiane na zama hizi, na wakazidi katika kosa hili kijumla na kivipande. Waka-stanbiti qaida za kijumla na hukmu za kivipande zinazowafikiana na mtazamo huo pindi walipoweka qaida za kijumla za kimakosa tofauti tofauti kwa mfano: (Haikatazwi kubadilisha hukmu kwa kubadilika wakati) na mfano: (Ada ndio zinazohukumu) na nyenginezo. Wakafutu kwa ahkamu zisizokuwa na mategemeo katika Sheria bali wakafutu kwa ahkamu zinazogongana na dalili ya kukatikiwa ya Qur'ani. Wakahalalisha riba kwa huja kwamba sio ya mara mbili mbili, na kwa hoja ya udharura kwa mali ya asiyebalighi, na akawa kadhi aliyeitwa (Kadhi wa Sheria) akihukumu na riba katika akiba ya mayatima kama yule kadhi aliyeitwa (Kadhi nidhamu) akihukumu na riba pia. Wakafutu kwa kusimamishwa hududi na wakaruhusu kuchukuliwa kanuni za kuadhibu wahalifu kwengineko kusokuwa Uislamu. Hivi ndivyo walivyoweka hukmu zinazokhtalifiana na Sheria kwa hoja yakuwa zawafikiana na zama, na udharura ya kuwafikiana Sheria na kila zama, wakati na mahali; na natija ya hayo ni kuweka Uislamu mbali na maisha. Wakatumia maadui wa Uislamu, kupitia ufahamu huu ulio changanyikiwa na hukmu hizi za kibatili, chombo cha kuwaingizia Waislamu kanuni zao na mifumo yao bila ya kuhisi Waislamu mgongono wowote na dini yao kwa sababu ya yaliyo kita katika fahamu zao, kwa ajili ya ufahamu ulio changanyikiwa kwamba Uislamu huwafikiana na kila wakati na mahali. Ukawa kutaawili Uislamu kwa ulimi wa wengi ili uwafikiane na kila madhabu, mfumo, tukio na msingi (*qaida*) hata kama hukhtalifiana na mfumo wa Kiislamu na mtazamo wake. Hii ilichangia kuweka Uislamu mbali na maisha, kwa hivyo ilikuwa ni jambo la lazima kushindwa kwa kila harakati ya marekebisho inayopelekwa kwa mujibu wa ufahamu huu wa kigonjwa.

Na ikaongezwa juu ya hilo katika mwanzo mwa karne ya ishirini kilicho makinisha vizuizi zilizosimama baina ya Uislamu na maisha, na kuzidisha juu ya taabu zilizosimama mbele ya harakati za Kiislamu taabu nyengine. Na hili ni kuwa Waislamu, khasa khasa wanavyuoni wa wanafunzi, walizidiwa kwa wakatu huu ya mambo matatu:

La kwanza yake ni kuwa walikuwa wakiufundsha Uislamu kwa njia inayokhtalifiana na njia ya kufundishwa kwake katika kuufahamu kwa sababu njia ya kuifundisha Uislamu ni kuzifundisha hukmu za ki-Sheria kama mas'ala ya kivitendo ya kutabikishwa na serikali kwa yale yanayo husika nayo, na kwa upande wa kibinafsi kwa mambo yanayo husikana na yeye. Kwahilo waliijua wanavuoni kwamba *fiqhi* ni: "Elimu (ujuzi) ya mas'ala ya ki-Sheria ya ki-vitendo yaliyovuliwa kutokamana na dalili fafanuzi." Kwa hilo huwa mafundisho yamezaa matunda ya ki-elimu, na kivitendo kwa mujtama katika serikali na kwa watu binafsi. Isipokuwa wajuzi na wanafunzi hawa, bali aghlabu ya Waislamu waliusoma Uislamu kwa mujarad ya elimu ya ki-nadharia kama kana kwamba ni falsafa ya ki-nadharia inayowazwa. Kwa hivyo zikawa hukmu za kifiqhi za ki-mawazo si zenye kutendwa. Na ikawa Sheria ni yenye kufundishwa kama ma'sala ya kiroho na ki-akhlaqi na sio hukmu za kutatua matatizo maishani. Huu ni kwa upande wa kufundisha. Amma kwa upande wa kulingania Uislamu, ikawa imeathiriwa na njia za ki-mawaidha na uongofu unaofwatwa na wa mishinari sio kwa njia ya kufundisha inayotakikanwa na Uislamu. Kwa haya wakawa wajuzi katika Uislamu ni imma wanavyuoni waliolala kana kwamba wao ni vitabu vinavyozunguka au imma ni watoaji mawaidha na uongofu wanao wakariria watu maneno (khutba) matupu bila yakuwa na athari yeyote katika mujtama. Wala hawafahamu maana ya thaqafa ya Kiislamu ambayo humaanisha kuwafundisha Waislamu mambo ya dini yao mafundisho yanao athiri hisia zao na kuwakhofisha na adhabu ya Allah na ghadhabu zake mpaka awe Mwislamu na nishati inayoathiri pindi inapounganishwa hisia zake na akili yake. Hayo ni kupitia kufundishwa kwa aya za Allah na kwa njia ya

kufundishwa kwake. Ndio hawakufahamu hilo, na wakaweka badala ya njia ya kufundisha inayoathiri ya ki-ndani, njia ya mawaidha na uongofu ambayo hufungika katika maneno (khutba) matupu. Ikawa kupitia hayo waliona kuwa baina ya kutatua matatizo ya mujtama na baina ya dini ya Kiislamu kuna mgongano au unaofanana na mgongano inayohitaji muafaka mpaka ikawa kufasiriwa Uislamu ili iwafikiane na zama ni jambo linalo kubalika kwa watu. Na juu ya hilo, walifahamu vibaya kauli yake ta’ala:

**{ وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا كَافَّةً فَلَوْلاَ نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِنْهُمْ طَائِفَةٌ لِيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ وَلِيُنْذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ } (التوبة: 122**

“*Wala haiwapasii Waislamu wote kutoka, Lakini kwa nini halitoki kundi katika kila taifa miongo mwao ili kusoma vizuri dini na kuwaonya wenziwao watakapo warudia ili wapate kujitahadharisha*”[TMQ 9:122].

Wakafasiri kutoka kutafuta elimu kutoka kila kikundi kipote kinacho jifundisha dini na kisha kurudi kuwafundisha wato wao. Kwa hivyo wakafanya kujifundisha dini ni fardhi ya kujitosheleza (*fardh kifaya*) na kwa hilo wakakhalifu hukmu ya ki-Sheria kama walivyokhalifu maana ya aya.

Amma hukmu ya ki-Sheria, nayo ni wajibu kwa kila Mwislamu aliyebalighi na mwenye akili ajifundishe katika dini mambo yanayomlazimu maishani kwa sababu yeye ni mwenye kuamrishwa kupeleka maisha yake yote kwa maamrisho ya Allah na makatazo yake. Na hakuna njia ya kufikia hilo ila kwa kujua hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na vitendo vyake; kwa hayo huwa kujifundisha katika dini kwa ahkamu za lazima kwa Mwislamu maishani ni fardhi ya kibinafsi (*fardh ‘ayn*) sio fardhi kifaya; amma ijtihadi kuvua (*istinbat*) ahkamu, hino ni fardhi kifaya. Amma kukhtalifiana kwao kwa maana ya aya, hakika ya aya ni aya ya jihadi. Nayo humaanisha kuwa haijuzu kwa Waislamu kutoka wote katika jihadi; litoke kikundi kwa ajili ya jihadi na libakie pote linalojifundisha hukmu kwa Mtume (SAAW) mpaka wanaporegea mujahidina hufundishwa

na waliobakia yaliyowapita katika hukmu za Allah mafundisho yanayoathiri fahamu zao. Na pia dalili juu ya haya ni waliokwako wakifuata masahaba (RAA) katika kujifundisha hukmu za dini na kujilazimisha kwao kwa Mtume (SAAW). Walikuwa baadhi yao wakitoka kwa vikosi vya jihadi na kubakia wanaobaki ili wajifundishe ahkamu za dini kisha wanaporudi mujahidina hufundishwa na waliobakia yale yaliowapita katika hukmu.

Ya pili yake ni kuwa mmagharibi hasidi anayechukia Uislamu na Waislamu aliuhujumu dini ya Kiislamu, akawa aki-udunga kisu na kuuzulia kwa upande na kwa upande mwengine hufanya zionekana kwa ubaya baadhi ya hukmu zake pamoja na kuwa ndizo utatuzi sahihi za matatizo maishani. Wakawa Waislamu khasa khasa waliowajuzi na msimamo mbele ya hujuma hii iliozidiwa na udhaifu pindi walipokubali Uislamu uwe ni mwenye kutuhumiwa na wakawa wenye kuutetea mpaka wakavutwa na haya kufanya majaribio ya kufasiri hukmu za Kiislamu. Kwa mfano wakatafsiri jihadi kuwa ni vita vya kujitetea sio kuhujumu. Kwa hilo wakakhalifu uhakika wa jihadi pamoja na kuwa jihadi ni vita na kila mwenye kusimama mbele ya ulinganizi wa Kiislamu sawa sawa awe ni mwenyu kuonyesha uadui au la. Kwa lugha nyengine ni kuondoa kila kikwazo kinacho simama mbele ya da’wa ya Kiislamu au ndio ulinganizi wa Uislamu na kupigana katika njia yake yaani katika njia ya Allah. Waislamu pindi walipohujumu Ufursi, Rumi, Masri, kaskazini mwa Afrika, Andalus na kwengineko hawakuhujumu ila kwa sababu ulinganizi unahitaji jihadi ili kuuneza katika biladi hizi. Kwa hivyo taawili hiyo juu ya jihadi ni kosa ambalo ni natija ya udhaifu wa kukubali Uislamu utuhumiwe na kutetewa kwake na utetezi unaodhihirisha kuwaridhisha wanaotuhumu. Na mfano wa haya ni suala la kuoa wake wengi, suala la kukata mkono wa mwizi na mengineo katika mas’ala waliojaribu Waislamu kuwajibia makafiri; wakakwa wanajaribu kuutawili Uislamu taawili inayogongana nayo. Na ikawa natija ya kupitia yote hayo ni kuwekwa

Waislamu mbali na kuufahamu Uislamu, na moja kwa moja kuwekwa mbali Uislamu mbali na kutendwa kazi.

Ya tatu yake ni kwa sababu ilopokuwa serikali ya Kiislamu ikilika kivuli chake (utawala wake) kutoka ma-eneo mengi ya Kiislamu na kunyenyekea kwake kwa hukmu za kikafiri, na kisha kuvunjika kwa serikali ya Kiislamu na kumalizwa kwake basi ikapatikana katika fahamu za Waislamu umuhali wa kuwepo serikali ya Kiislamu na umuhali wa kuhukumu kwa Uislamu peke yake. Kwa hivyo walikuwa wakiridhika kuhukumu kinyume na aliyoyateremsha Allah, wala hawaoni kosa katika hili maadamu imehifadhiwa jina la Uislamu hata kama haihukumu nayo. Na wanalingania uwajibu wa kustafidi na madhehebu na mifumo mengine ili zisaidie kwa utabikishaji wa Uislamu maishani. Natija ya haya ni kuwacha kazi ya kuregesha serikali ya Kiislamu na kunyamaza juu ya kutabikishwa hukmu za kikafiri juu ya Waislamu kwa mikono ya Waislamu.

Ikawa kwa sababu zilizotangulia kuzoroteka harakati zote za kutengeneza zilizo simama kuwapa Waislamu mwamko na kurudisha jaha ya Uislamu; ikawa ni kawaida kuzoroteka kwa sababu yake. Na hata kama zilikuwa harakati za Kiislamu, lakini zilikuwa na ufahamu baya juu ya Uislamu lililozidisha tatizo na mushkila kuwa mgumu na kuuweka mujtama mbali na Uislamu badala ya kufanya kazi ili kuitabikisha juu yake.

Kwa haya ilikuwa hapana budi kuwa na harakati ya Kiislamu inayofahamu Uislamu, fikra na twarika, na kuunganishia baina yake na kufanya kazi ili kurudisha maisha ya Kiislamu katika eneo miongoni mwa ma-eneo ya Kiislamu mpaka uwe eneo hilo ni nukta ya kuanzia inayochimbuka kutokana nayo ulinganizi wa Kiislamu kisha iwe ni nukta ya kusongea mbele kwa ulinganizi wa Kiislamu.

Juu ya msingi huu, imebuniwa Hizb ut-Tahrir na ikasimama kufanya kazi ili kurudisha maisha ya Kiislamu katika biladi za

kiarabu na itakuwa natija yake—ya kutarajiwa kikawaida—ni kurudisha maisha ya Kiislamu katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kuweko serikali ya Kiislamu katika eneo au ma-eneo kama nukta ya kusimamisha Uislamu, na kiini cha serikali kubwa ya Kiislamu, ambayo itarudisha maisha ya Kiislamu kwa kuutabikisha Uislamu na kubeba ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu wote.

Baada ya kusoma, fikra na uchunguzi imetabanni Hizb ut-Tahrir hii hukmu za ki-Sheria, baada zinaambatana na utatuzi wa matatizo ya ki-binafsi ambayo hutokea baina ya watu na katika mafungamano baina watu na watu wenziwao mfana kuzuia kukodisha ardhi kwa ajili ya ukulima. Na miongoni yake ni yale yanayoambatana na rai jumla inayotukia baina ya Waislamu jumla na wengineo katika mafungamano ya Waislamu jumla na wengineo na katika mafungamano ya Waislamu jumla na wengineo mfano kuruhusiwa mikataba ya kidharura na ulinganizi kwa Uislamu kabla ya kuanza vita na yanayoshabihiyana nayo. Na miongoni yake ni yale yanayoambatana na fikra nazo ni ahkamu za Sheria kama hukmu nyenginezo za ki-Sheria na hizo ni kama qaida za kijumla na istilahi mfano: ‘Kisicho timia wajibu ila kwayo basi hiyo ni wajibu’ na mfano istilahi ya hukmu za Sheria kuwa ni khutuba ya mtungaji Sheria yanayo ambatana na vitendo vya waja, na yanayo shabihiyana nayo. Hakika imetabanni Hizb katika kila sampuli katika sampuli hizi miongoni mwa hukmu, hukmu maalumu na ikawa inazilingania inapolingania kwa Uislamu. Na hizi ni rai, fikra na hukmu za Kiislamu si nyengine na hazina ndani yake kitu chochote kisicho kuwa cha Kiislamu wala hazi-athiriki na kitu chochote kisichokuwa cha Kiislamu bali ni za Kiislamu tu zisiotegemea tofauti na misingi na dalili za Kiislamu. Na hutegemea Hizb ndani yake juu ya fikra na huona kuwa ulinganizi kwa Uislamu ni lazima usimame juu ya fikra na ibebwe kama fikra kiongozi kwa sababu fikra ya ki-ndani iliokamilika ndio inayosimama juu yake maisha na ndiyo ndio inayomwendeleza mwanadamu kwa msingi wake. Na ndiyo inayoonyesha uhakika wa vitu vikadirikiwa udiriki ulio

sahihi. Na fikra mpaka iwe ya ki-ndani iliyokamilika haina budi ila iwe ya ki-ndani na fikra ya ki-ndani ni mtazamo wa ki-ndani juu ya vitu. Na fikra ya ki-ndani iliyokamilika ni mtazamo wa ki-ndani juu ya vitu na hali zake na yanayoambatana nayo na kustadili kwa hayo ili kufikia kwa natija ya kikweli. Na kwa maana nyengine ni mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya vitu kwa hivyo hakuna budi ila kuwepo mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu na hakuna budi ila kuwepo mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya mwanadamu na vitendo vya mwanadamu ili imkinike kudiriki hukmu zinazofungamana juu yake.

Na mtazamo wa ki-ndani juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai ndio unaotoa kutokamana nayo fikra jumla (*fikra kuliyya*) na ndio inayotatua tatizo kubwa kwa mwanadamu na ndio huwa ni aqeeda kwa mwanadamu na ndio inay-muwekea mwanadamu lengo la maisha na lengo la vitendo anayoyatenda maishani. Kwa sababu mwanadamu huishi ulimwenguni na ikiwa halijatatuka tatizo kubwa katika nafsi yake na juu ya uhai anayoishi ndani yake na juu ya ulimwengu ambayo ni mahala pa maisha yake na kuwepo kwake wala haimkiniki kujua suluki ambazo yampasa azifuate kwa hivyo imekuwa aqeeda ndio msingi wa kila kitu.

Na mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai hufikisha kwa aqeeda ya Kiislamu inayodhihirisha kwa uwazi kuwa hizo ni viumbe vilivyo umbwa na muumba na kuwa muumba huyu ndiye peke yake anavyoviendesha na husimama kwa kuzihifadhi na kuziendesha kwa nidhamu mahsusan. Na kuwa maisha haya na dunia sio ya kudumu wala si ya milele. Hupatikana aliyoko kabla yake nayo ni muumba wake na mwendeshaji wake na hupatikana kilicho baada yake nayo ni Siku ya Qiyama na kuwa vitendo vya mwanadamu katika maisha haya ya dunia ni lazima yapelekwe kwa mujibu ya maamrisho ya Allah na makatazo yake. Na kuwa mwanadamu atahisabiwa juu yake Siku ya Qiyama nayo ni Siku ya Hisabu. Kwa hivyo huwa ni lazima kwa mwanadamu

kujifunga na Sheria ya Allah ambayo imefikishwa kwake na Mtume wa Allah, bwana Muhammad (SAAW).

Na mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu huonyesha kuwa ni mada tu sio roho wala hakuundwa kutokamana na mada na roho. Maana ya mada hapa ni kitu kinacho dirikiwa kinacho hisika, sawa sawa kijulikane mada kama chenye umbo na uzito au kinachojulikana kama nguvu (*mashuna*) ya kidhahiri au kilichofichika. Uchunguzi hapa si juu ya ni nini mada bali uchunguzi bali ni juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu—haya mambo yanayo hisika na kudirikiwa—kwa upande wa kuwa vimeumbwa na muumba. Na maana ya roho hapa ni kudiriki fungamano na Allah sio maana ya siri ya uhai. Uchunguzi si juu ya roho kwa maana ya siri ya uhai bali uchunguzi ni juu ya fungamano la ulimwengu, uhai na mwanadamu kwa aliye ghaibu nayo yaani muumba, na juu ya kudiriki fungamano hili maana yake kudiriki fungamano la ulimwengu, uhai na mwanadamu kwa muuba wake ni sehemu yake au si sehemu yake.

Mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya ulimwengu, uhai na mwanadamu, kutoka upande wa maana ya roho kuwa ni kudiriki fungamano na Allah si upande wa roho kama siri ya uhai, huonyesha kuwa ni mada tu sio roho wala hakuundwa kutokamana na mada na roho. Amma kuwa ni mada ni wazi bila kuficha kwa sababu hudirikiwa na huhisiwa. Amma kuwa si roho hio ni kuwa roho ni mwanadamu kudiriki fungamano lake na Allah ta'ala ambayo kudiriki hivi mwanadamu fungamano lake na Allah si ulimwengu, mwanadamu wala uhai bali ni kitu chengine yasiokuwa hayo. Amma kuhusu kuwa hakuundwa kutokamana na mada na roho, hino ni wazi katika ulimwengu na uhai. Amma katika mwanadamu, hakika kudiriki kwake kwa fungamano na Allah si sehemu la umbile/muundo bali ni sifa ya ziada kwa dalili ya kuwa kafiri anayekanusha kuwepo Allah hadiriki fungamano lake na Allah na pamoja na hilo ni mwanadamu.

Na kwa haya, hakika yale wanayo yasema baadhi ya watu ya kuwa mwanadamu ameundwa kutokamana na mada na roho, na inaposhinda ndani yake mada juu ya roho huwa ni mwovu na inaposhinda ndani yake roho juu ya mada huwa ni mwema na ni jukumu lake kufanya roho ishinde juu ya mada ili awe ni mwema. Msemo huu sio sahihi; mwanadamu hakuundwa juu ya mada na roho na hilo ni kwa sababu roho inayochunguzwa katika mlango huu katika watu wote wanao amini kuwepo muumba ni athari ya muumba au kinacho shuhudiwa miongoni mwa athari katika upande wa yaliyofichika au kuwa kitu kinachodirikiwa ndani yake kuwa hakikupatikana ila kutoka kwa Allah au kwa maana hino ni uroho au upande wa kiroho. Na roho kwa maana ya uroho au upande wa kiroho inayopatikana kwa mwanadamu sio siri ya uhai wala haitokamani na srii ya uhai wala haina mafungamano ya siri ya uhai bali ni kitu chengine tofauti kwa dalili kuwa hayawani ana siri ya uhai na pamoja na hilo haina uroho wala upande wa kiroho, wala hakuna yeyote anayesema kuwa yeye (hayawani) ameundwa juu ya mada na roho hali inayoleta yakini kuwa roho kwa maana hii sio siri ya uhai wala haitokamani na siri ya uhai wala haina mafungamano na siri ya uhai. Kaaa alivyokuwa hayawani hakuundwa juu ya mada na roho pamoja na kuwa ana siri ya uhai, hivyo hivyo mwanadamu hakuundwa juu ya mada na roho hata kama anayo ndani yake siri ya uhai kwa sababu roho inayomtofautisha mwanadamu na inayopatikana kwake haifungamani na siri ya uhai wala haitokamani nayo bali ni tu kudiriki fungamano na Allah, basi haisemwi kuwa ni sehemu ya muundo ya mwanadamu kwa hoja ya kuwa ana siri ya uhai.

Na madamu roho inayochunguzwa hapa katika mlango huu ni kudiriki fungamano na Allah wala haina fungamano na siri ya uhai, kwa hivyo haiwi ni sehemu ya muundo wa mwanadamu kwa sababu kudiriki fungamano sio sehemu ya muundo wake bali ni sifa ya ki-inje kwa dalili ya kuwa kafiri anayekanusha kuwepo Allah hadiriki fungamano lake na Allah na pamoja na hilo yeye ni mwanadamu.

Pamoja kuwa ulimwengu, mwanadamu na uhai ni mada wala sio roho lakini upande wake wa kiroho ni kuwa ni viumbe vilivyo umbwa na muumba maana yake hiyo ndio fungamano zao, kwa sifa zao kama viumbe, na Allah ta'ala muumba wao. Ulimwengu ni mada na hali yake kama kiumbe kilicho umbwa na muumba ndio upande wa kiroho ambacho hukidiriki mwanadamu na mwanadamu. Na uhai ni mada na hali yake kama kiumbe kilicho umbwa na muumba ndio upande wa kiroho ambacho hukidiriki mwanadamu. Upande wa kiroho haitokamani na dhati ya ulimwengu au uhai au mwanadamu bali ni hali ya kuwa viumbe cha muumba aliyeviumba naye ni Allah ta'ala. Fungamano hili ndilo upande wa kiroho.

Na asli katika maana ya roho ni kuwa watu ambayo huamini kuwepo mungu hurudia matamko ya roho, uroho na upande wa kiroho na hukusudiwa kutokamana nayo athari ya muumba katika mahali au kinacho shuhudiwa katika upande wa *ghaibu* au hali ya kudirikiwa katika kitu kisichotokea ila kutoka kwa Allah au kwa maani hii. Maana hizi huitwa kwayo roho, upande wa kiroho na uroho au kwa maana hizi, maana jumla ziliofichika zisioeleweka zisiokuwa wazi. Hizi zina hakika ndani ya fahamu zao na zina hakika nje yao nayo ni *ghaibu* inayodirikiwa kuwepo kwake isiodirikiwa dhati yake na athari ya *ghaibu* katika vitu, lakini uhakika huu ambayo wanaouhisi hutukia kivitendo katika hisia zao lakini wao hawawezi kuijua kwa sababu si wazi kwao wao. Ikawa kwa sababu ya kutokuwa wazi kwao maana hizi kwamba ilichanganyikiwa sura yake kwao, basi ikachangayikiwa kwa baadhi yao kuwa ni roho ambayo ni siri ya uhai, wakawa wanamsema mwanadamu kuwa ameundwa kutokamana na mada na roho kwa sababu ya kuhisi kwao kuwepo roho ambayo ni siri ya uhai na kuwepo roho kwa maana ya uroho au upande wa kiroho wakadhania kuwa haya ndio yale au kuwa zimetokamana na yale wala hawakutazama hayawani aliye na roho maana yake siri ya uhai wala hana uroho au upande wa kiroho. Na pia ilikuwa kutokamana na kutokuwa wazi kwao wakaanza kuita kila kinacho patikana kutoka kwa mwanadamu katika jadhba ya kinafsi kuwa ni uroho; husema

mtu juu ya nafsi yake kuwa anahisi uroho wa hali ya juu au fulani ana uroho mkubwa. Na ikawa pia kutokamana na kutokuwa wazi kwao wakawa wakenda mahali na kuhisi hapo utulivu au msisimko kisha kusema mahala hapa mna upande wa kiroho au uroho. Na ikawa pia kutokamana na kutokuwa wazi kwao akawa mtu akiiweka na njaa nafsi yake, kuutesa mwili wake na kuukondesha mwili wake akidai kuwa yeye anataka kuitia nguvu roho yake. Yote hayo ni kwa sababu ya kutokuwa wazi kwao maana ya roho, maana ya uroho na maana ya upande wa kiroho. Hayo hushabihiyana na uhakika wa akila kwa waliotangulia. Hakika akili ni tamko linalokusudiwa kutokamana nalo utambuzi/udirikaji na hukmu/uamuzu juu ya kitu na yaliyomo katika maana hii lakini waliotangulia walikuwa wakiona kuwa vitu hivi miongoni mwa utambuzi na nyengine ni athari ya akili sio akili yenyewe. Na kwao wao akili ni hakika wanao uhisi lakini hawajabainikiwa uhakika wake nayo si wazi kwao. Na kwa sababu ya kutokuwa wazi kwao wao, ulikhtalifiana mtazamo wao kwake na kugongana mtazamo wao juu ya mahala pake na wakachanganyikiwa katika kudiriki wake na uhakika wake. Miongoni mwao wanasema iko katika moyo na miongoni mwao wanasema kuwa iko katika kichwa na miongoni mwao wapo wanaosema kuwa iko katika ubongo na wapo miongoni mwao wanaosema mengineyo. Na zilipokuja zama hizi, wakajaribu baadhi ya mufakirina kuweka wazi maana ya akili na kuijua; wakadanganyika kwa kukosa kudiriki uhakika wake. Wakasema baadhi yao kuwa ni athari ya ubongo juu ya mada na wakasema wengineo kuwa ni athari ya mada juu ya ubongo, mpaka ili tambulikana utambuzi sahihi kuwa ni kunukuliwa uhakika (*waqi'ah*) mpaka katika ubongo kupitia hisia na maalumuti zilizotangulia zinazofasiri uhakika huo. Na kwa utambuzi huu ilidirikiwa ni nini akili. Na hivyo hivyo hakuna budi kwa baadhi ya mufakirina ila kufafanua uwazi maana ya roho, uroho na upande wa kiroho na yaliyomo katika maana ya haya, uwazi inayofanya fahamu kuzidiriki na kudiriki uhakika yake kwa sababu kuna uhakika kwa roho, uroho na upande wa kiroho kinacho shuhudiwa na kuhisiwa na mwanadamu. Hino ni kwa sababu kuna vitu vya ki-mada anavyo

vihisi mwanadamu na huenda akazishika kama mkate, na huenda kuzihisia wala asiweza kuzishika kama huduma za tabibu. Na kuna vitu za ki-*ma'nawiya* anavyo vihisi wala hawezi kuzishika kama ufahari na sifa. Na kuna vitu vya kiroho anavyo vihisi wala hawezi kuzishika kama kumcha Allah na kusalimu amri kwake wakati wa shida. Maana hizi tatu zina uhakika anazo zihisi mwanadamu na kutofautika moja wapo kutoka nyenginezo na huwa roho au upande wa kiroho au uroho ni hakika maalumu inayotukia hisia juu yake basi hapana budi ili kuzitambua hakika hizi ili kuziweka wazi kwa watu kama ilivyo tambulikiwa akili na kuwekwa wazi kwa watu.

Uchunguzi katika hakika ya roho, uroho na upande wa kiroho hubainisha kuwa haupatikani kwa (*mulhid*) mwenye kukanusha kuwepo Allah na kuwa hupatikana tu kwa wanaoamini katika kuwepo mola. Na hii humaanisha kuwa imefungamana kwa imani juu ya Allah, hupatikana mahala panapo patikana imani hii na huadimika inapo adimika. Na imani ya kuwepo Allah maana yake ni kusadikisha kuliko katikiwa kuwa vitu ni viumbe vilivyoumbwa na muumba. Na huwa maudhui ya uchunguzi ni kuwa vitu vya hali vyao kuwa viumbe vya muumba; kukiri kuwa vimeumbwa na muumba ni imani, na kukanusha kuwa vimeumbwa na muumba ni ukafiri. Katika hali ya kukiri na kusadikisha kuliko katikiwa hupatikana upande wa kiroho, na ambalo kimeileta ni kusadikisha. Na katika hali ya kukosekana kukiri na kukanusha haupatikani upande wa kiroho, na ambalo kilichofanya kutopatikana ni kukanusha. Basi huwa upande wa kiroho ni kile vitu vimeumbwa na muumba yaani ni fungamano wa vitu na muumbao wao kwa upande wa kuumbwa na kuundwa kutoka hali ya kutokuwepo. Fungamano hili, yaani kuwa vimeumbwa na muumba, inapodirikiwa na akili hupatikana kupitia kudiriki huko hisia kwa ukubwa wa muuba na hisia ya kumcha yeye na hisia ya kumtukuza; huwa kudiriki huku ndio inayozalisha hisia kwa fungamano hili nayo ni roho. Basi huwa roho ni kudiriki fungamano na Allah. Na kwa hayo huwa wazi maana ya upande wa kiroho na maana ya roho, nayo sio matamko yaliyo na maana ya ki-lugha ambayo huregelea

maana yake kutokamana na lugha wala sio istilahi ambayo kila watu wawe na istilahi zao kama wanavyotaka wao. Bali na maana zilizo na uhakika maalumu vyovyote zitakavyo bandikiwa majina. Uchunguzi huwa ni juu ya uhakika na maana hizi sio maana la tamko la ki-lugha; uhakika wa maani hizi ni huu nayo ni kuwa roho inayolingana na upande wa kiroho katika mwanadamu ni kudiriki fungamano na Allah. Na upande wa kiroho katika ulimwengu, mwanadamu na uhai ni kule kuwa ni viumbe vilivyoumbwa na muumba. Vyovyote litakavyo bandikwa tamko hilo huwa makusudio yake ni kwa maana hii kwa sababu ndio uhakika unaohisia na iliyosimama dalili ya kukatikiwa juu yake. Na kwa kuwa uhakika huu unaohisiwa ndio uhakika wa ki-ndani na wa ki-nje kwa mtu anayeamini kuwepo mola yaani kuwepo muumba wa vitu.

Amma roho ambayo ni siri ya uhai nayo kuwepo kwake hakuna shaka na imethubutu kwa dalili ya kukatikiwa ya Qur'ani, na imani juu ya kuwepo kwake ni jambo la lazima nayo sio maudhui wa uchunguzi huu.

Na tamko la roho (*ruh*) ni tamko lililobeba maana nyingi kama *'ayn* inayobeba maana nyingi. Kama ilivyokuwa *'ayn* ni jina liitwalo vitu vyingi kama kuitwa mto, jicho, jasusi, dhahabu, fedha na mengineo, hivyo hivyo *ruh* huitwa maana nyingi. Imethubutu katika Qur'ani kwa maana nyingi. Imekuja *ruh* kwa maana ya siri ya uhai:

**{ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلاَّ قَلِيلاً } (الإسراء: 85)**

"*Wanakuuliza juu ya roho, Sema: 'Roho ni jambo lililohusika na Mola wangu wala hamukupewa katika elimu ila kidogo'*" [TMQ 17:85]. Na imekuja kwa maana ya Jibril (AS):

**{ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الأَمِينُ - عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنْ الْمُنذِرِينَ }(الشعراء: 193- 194**

"*Ameteremka nayo roho mwaminifu.Juu ya moyo wake, ili uwe miongoni mwa waonyaji*" [TMQ 26:193-194]. Na imekuja kwa maana ya Sheria:

**{ وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِنْ أَمْرِنَا } (الشورى: 52**

"*Na kadhalika Tumekufunulia kwa wahyi roho kutoka amri Yetu*"[TMQ 42:52].

Na maana haya yote sio yanayokusudiwa katika msemo huu wa upande wa kiroho au kitu cha kiroho au kutenganisha mada na roho au yanayoshabihiyana nao. Wala hakuna mahusiano katika kauli juu ya roho na maana ya roho yaliyothubutu katika Qur'ani bali maana iliyokusudiwa juu ya roho katika matamshi haya ya mwisho ni maana iliyofungamana na kuumbwa mada yaani kwa upande wa kuwa vitu vimeumbwa na muumba nayo ni Allah ta'ala na kudiriki kwa mwanadamu fungamano la vitu kwa muumba wake.

Na mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya mwanadamu huonyesha kuwa yeye anaishi katika mizunguko miwili: La kwanza lake ni ule unaomtawala yeye ya la pili lake ni ule anaoutawala yeye. Amma ambao unaomtawala yeye ni mzunguko ambayo ndani yake unatabikishwa nidhamu za ki-maisha basi yeye hupelekwa pamoja na ulimwengu na uahi kwa mujibu wa nidhamu maalumu isiyobadilika. Kwa hivyo hutukia vitendo juu yake katika mzunguko huu bila ya matakwa yae, na yeye huishi ndani yake bila kukhiyarishwa. Hakika yeye ameletwa katika dunia hii bila ya matakwa yake na ataiondoka bila ya matakwa yake, na yeye hamiliki uweza wa kutoka kwenye nidhamu ya ki-ulimwengu. Na kwa hivyo hataulizwa juu ya vitendo vinavyotokamana na yeye na juu yake katika mzunguko huu. Amma mzunguko ambao huutawala yeye nao ni mzunguko ambao yeye huenda ndani yake kwa khiyari kwa mujibu ya nidhamu anayoichagua sawa sawa iwe Sheria ya Allah au nyengineo. Katika mzunguko huu, hutukia ndani yake vitendo ambavyo hutokamana na mwanadamu au juu yake kwa matakwa yake. Yeye hutembea, hula, hunywa na husafiri katika wakati wowote autakao na hujizuia na hayo katika wakati wowote autakao. Hutenda kwa khiyari na hujizuia kwa khiyari kwa hivyo huulizwa juu ya vitendo anavyo vitenda katika mzunguko huu.

Na yeye—yaani mwanadamu—hupenda vitu vinavyotokamana na yeye au juu yake katika mzunguko unaomtawala yeye na anaoutawala yeye, na huchukia vitu katika mizunguko hayo. Na hujaribu kufasiri mapenzi haya na chuki hizi kuwa kheri na shari. Na huelekea kuita kila anacho kipenda kuwa ni kheri na anacho kichukia kuwa ni shari. Hivyo hivyo huviita vitendo kuwa ni kheir na vitendo vyengine kuwa ni shari kwa msingi wa kufikiwa kwake manufaa kutokamana navyo au kugusiwa na madhara kutokamana navyo.

La uhakika ni kuwa vitendo ambavyo hutukia kutoka kwa mwanadamu katika mzunguko wake haijulisha kwa dhati yake kuwa ni kheri au shari kwa sababu hivo ni vitendo tu mujarad visivyo na sifa yeyote kwa dhati yake kuonyesha kuwa ni kheir au shari. Bali huwa kheri au shari huja tu kwa msingi wa hisabu ya ki-nje juu ya dhati ya vitendo. Kuuwa nafsi ya mwanadamu hauitwi kheri au shari bali huitwa tu mauaji. Kuwa kheri au shari huja tu kwa sifa nje yake inayokuja juu yake. Kwa hivyo huwa kumuua mpiganaji ni kheri na kumuua mraia au aliye na ahadi (*mu'ahid*) au aliyepewa amani (*musta'man*) ni shari. Hutuzwa muuwaji wa kwanzo na huadhibiwa muuwaji wa pili pamoja na kuwa kitendo chao ni kimoja bila tofauti yeyote. Lakini kheri na shari hutokamana na sababu zinazompelekea mwanadamu katika kutenda kitenda na lengo analolilenga katika kutenda kitendo hicho. Sababu zinazompelekea mwanadamu kutenda kitendo na lengo analolilenga ndani yake ndizo sababu mbili zinazoweka sifa za kitenda kuwa ni kheri na shari sawa sawa amependezwa mwanadamu au kuchukuzwa na sawa sawa amepata manufaa au madhara.

Na kwa haya imekuwa lazima kuchunguzwa sababu/dhurufu zinazompeleka mwanadamu kutenda kitendo na kuchunguzwa lengo ambalo hulilenga na wakati huo itafahamika lini kitendo husifiwa kuwa ni kheri au shari. Na kuzijua dhurufu zinazompeleka na lengo analolilenga hutegemea aina ya aqeeda anayoitakidi mwanadamu. Basi Mwislamu ambaye amwamini Allah na kuamini kuwa Yeye ndiye aliyemtumiliza bwana

Muhammad (SAAW) na Sheria ya Kiislamu inayobainisha maamrisho ya Allah na makatazo Yake, na kupanga mahusiano yake na Mola wake na nafsi yake na watu wengineo: Ni lazima Mwislamu huyu kupeleka mambo yake kwa mujibu ya maamrisho ya Allah na makatazo Yake, na liwe lengo analolilenga katika mambo yake ni kunali radhi za Allah. Kwa hivyo huwa kitendo husifiwa kuwa cha kumghadhibisha Allah au kumridhisha; ikiwa ni yenye kumghadhibisha Allah kwa hukhtalifiana na maamrisho Yake na kufuata makatazo Yake huwa ni shari, na ikiwa ni yenye kumridhisha Allah kwa kutii maamrisho Yake na kuepukana na makatazo Yake huwa ni kheri.

Kwa hayo twaweza kusema: Kheri kwa mtazamo wa Mwislamu ni kila kinachomridhisha Allah na shari ni kila kinachomghadhibisha.
Na haya hulingana na vitendo vinavyo tokamana na mwanadamu au juu yake katika mzunguko anaoutawala.

Amma vitendo vinavyo tokamana na mwanadamu au juu yake katika mzunguko unaomtawala yeye, mwanadamu huzisifu na kheri au shari kufuata mapenzi yake au kuchukia kwake au kunufaika kwake au kudhurika kwake:

**{ إِنَّ الإِنسَـانَ خُلِـقَ هَلُوعًـا ـ إِذَا مَسَّـهُ الشَّـرُّ جَزُوعًـا ـ وَإِذَا مَسَّـهُ الْخَيْـرُ مَنُوعًـا } (المعارج: 19 -21)**

"*Kwa hakika binadamu ameumbwa hali ya kuwa mwenye papatiko (pasina subra).Inapomgusa shari huwa mwenye fazaa (wasiwasi). Na inapomgusa kheri huwa anaizulia*" [TMQ 70:19-21] na:

**{ وَإِنَّهُ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ } (العاديات: 8**

"*Na ana mapenzi makubwa kabisa ya kupenda mali*" [TMQ 100:8].

Mtazamo wa ki-ndani uliokamilika juu ya vitendo vya mwanadamu huonyesha kuwa ni mada tu kwa asili ya dhati yake

ikiviluwa dhurufu na hisabu zote. Na hali yake kama mada kwa dhati yake haijulishi kama ni zuri (*hasan*) au baya (*qabeeh*) bali hujulikana kwa hayo kutokamana na dhurufu zake za ki-nje na kwa hisabu zinazotokamana na mengineo. Na huyu mwengine ambaye hubainisha kitendo kuwa ni zuri au baya imma iwe ni akili pekee au Sheria peke yake; au imma iwe ni akili na dalili yake iwe ni Sheria au Sheria na dalili yake iwe ni akili. Amma kuisifu kwa upande wa akili pekee, hino ni batili kwa sababu akili inasibiwa na udhaifu, kutofautiana, ikhtilafu na migongano basi vipimo vya akili kwa zuri na baya huathiriwa na mazingira anaoishi ndani yake bali hutofautika na kukhtalifiana kwa zama zinapobadilika. Na inapowachwa kipimo cha baya na zuri kwa akli huwa kitu ni kibaya kwa baadhi wa watu na zuri kwa wengine, bali huenda kikawa kitu kimoja kuwa ni kizuri katika zama na kibaya katika zama zengine. Uislamu kwa sifa yake kama mfumo wa ki-ulimwengu unaodumu milele hulazimu kuwa sifa cha kitenda kiwe kizuri au kibaya sawa sawa kwa wanadamu wote katika zama zote. Kwa hivyo hapana budi ila kubainishwa kitendo kuwa zuri au baya kutokamana na nguvu iliyo juu ya akili ikawa hapana budi ili itokamane na Sheria (*Ash-Shari'*). Kwa hivyo hino sifa ya kitendo cha mwanadamu kuwa baya au zuri hutokamana na Sheria na kufikia hapa imekuwa udanganyifu ni uovu na utekelezaji ahadi ni uzuri, na ikawa ufasiki ni uovu na uchaji mungu ni uzuri, na ikawa uasi dhidi ya serikali ya Kiislamu ni uovu na kusahihisha kuteleza kwake ikiteleza ni kitendo kizuri kwa sababu Sheria ishabainisha hayo. Amma kufanya Sheria dalili kwa iliodokezewa na akili, hino hulazimisha kufanya akili ni yenye kuhukumu katika zuri na baya na tumekwisha bainisha ubatili wake. Amma kuifanya akili ni dalili kwa iliodokezewa na Sheria, hino hulizimu kuifanya akili ni dalili juu ya humu ya ki-Sheria. Lakini dalili ya hukmu ya ki-Sheria ni *nasi* (msemo wazi wa ki-wahyi) sio akili, na jukumu la akili ni kufahamu hukmu ya ki-Sheria sio kuifanya dalili juu yake. Na kufikia hapa huwa zuri na baya ni kutokamana na Sheria tu sio akili.

Tofauti baina ya kusifu kitendo kuwa ni kheri (*khayr*) au shari (*sharr*) na baina kukisifu kuwa ni zuri (*hasan*) au baya (*qabeeh*) ni kuwa kuisifu kuwa ni kheri na shari huwa kwa sababu ya athari yake katika mtazamo wa mwanadamu na kwa sababu ya kuitangulia au kukipa nyongo. Mwanadamu huita kila kinachomdhuru au kukichukia miongoni mwa vitendo kuwa ni shari, na huita kila kinachomnufaisha na anachokipenda miongoni mwa vitendo kuwa ni kheri kwa sababu ya athari yake juu ya hilo bila kujua uzuri na ubaya hilo halipatikani kwake katika hali hii. Na kujengea juu ya mtazamo huu hutangulia kitendo au kukipa nyongo. Ikaja usahihishaji kwa mtazamo huu kuwa kitendo hakisemwi kuwa ni kheri au shari kwa mujibu wa kuchukiwa na kupendwa au manufaa na madhara, bali kipimo cha kuwa kheri au sheri ni kumridhisha Allah ta'ala. Huu ndio uchunguzi wa upande wa kipimo cha kheri na shari ambacho watu wamekitambua na sio kwa upande wa kitendo chenyewe.

Amma kusifu vitendo kuwa ni vizuri au vibaya, hii ni katika upande wa hukmu juu yake kutoka wa mwanadamu na kwa upande wa adhabu na thawabu. Hakika mwanadamu amejipa nafsi yake jukumu la kuhukumu kitendo kuwa ni kizuri au kibaya kama kipimo cha vitu. Alipokuta kuwa anaweza kuhukumu kitu kichungu kuwa ni kibaya na kitu kitamu ni kizuri na chenye muundo wa kutisha kuwa ni kibaya na chenye muundo mzuri kuwa ni kizuri, ameona kuwa anaweza kuhukumu juu ya ukweli kuwa ni uzuri na urongo kuwa ni ubaya na kutekeleza ahadi kuwa ni uzuri na khiyana kuwa ni ubaya. Akajipa nafsi yake jukumu la kuhukumu vitendo kuwa ni zuri au baya bila kuangalia maudhi ya kheri na shari hilo halipatikani kwao katika hali hii na kujengea juu ya hukmu yake hii ameweka adhabu juu ya vitendo vibaya na akaweka tuzo kwa kitendo kizuri. Likaja sahihisho kwa hukmu hii kuwa kitendo halipimwi juu ya kitu kwa sababu kitu kinachodirikiwa na hisia kwao ni chungu na tamu, cha kutisha au sura nzuri inayomwezesha kuhukumu, kinyume na kitendo kisichopatikana kitu ndani yake anachokihisi mwanadamu hata aweze kuhukumu kuwa ni kibaya au kizuri. Haimkiniki kata kata

kuvihukumu (vitendo) kuwa ni zuri au baya kwa nafsi yake basi hapana budi kuchukuwa hukmu hii kwa mwengine naye ni Allah ta'ala. Uchunguzi huu ni juu ya hukmu juu ya kitendo sio katika upande wa vipimo; na uchunguzu hapa ni kwa upande wa adahbu juu ya vitendo na thawabu zake sio kwa upande wa kuitangulia au kuipa nyongo. Kwa hivyo kuna tofauti baina ya kheri (*khayr*) na shari (*sharr*) na baina ya zuri (*hasan*) na baya (*qabeeh*), na umekuwa uchunguzi mbili mbali mbali kabisa.

Huu ni kwa upande wa kusifu vitendo. Amma katika upande wa kukusudia kitendo hapana budi kwa kila mwenye kutendo kitendo kuwa na makusudio ambao hutenda kwa ajili yake, na makusudio hayo ndio thamani ya kitendo. Kwa hivyo ni lazima kwa kila kitendo kuwa na thamani akilengacho mwanadamu kukihakikisha pindi anapotenda kitendo, na ikiwa hakina basi huwa ni mujarad wa ki-holela. Haistahiki kwa mwanadamu kutenda vitendo vyake ki-holela bila makusudio, bali hapana budi ila kuchanga kuhakikisha kwa thamani ya vitendo anavyokusudia kutenda kwa ajili yake.

Na thamani ya vitendo ni imma iwe thamani ya ki-mada kama vitendo vya ki-biashara, ukulima, usanii na mithali yake. Hakika linalo kusudiwa katika vitendo hivi ni kupatikana manufaa ya ki-mada kutokamano nazo nayo ni faida ambao ni thamani ilio na uzito wake maishani. Na imma iwe thamani ya kitendo ni utu kama kuokoa waliozama na kuwasaidi wahitaji. Hakika linalokusudia katika kumuoka mwanadamu bila kuangalia rangi yake, jinsiya yake, dini yake au hisabu yeyote nyengine isiokuwa uwanadamu. Na imma iwe thamani ya kitendi ni ya ki-akhlaqi kama ukweli, uaminifu na huruma. Hakika linalolengwa kutokamana nayo ni upande wa ki-akhlaqi bila kuangalia faida na bila kuangalia utu. Pia huenda ikawa akhlaqi pamoja na asiyekuwa mwanadamu kama upole kwa hayawani na ndege, na huenda ikapatikana kutokamana na kitendo cha akhlaqi hasara ya kimada lakini kuhakikisha thamani yake ni wajibu nayo ni upande wa ki-akhlaqi. Na imma iwe thamani ya kitendo ni uroho kama ibadati. Sio linalokusudiwa kutokamana nalo faida

ya ki-mada wale upande wa ki-utu wala mas'ala ya ki-akhlaqi bali linalokusudiwa kutokamana nalo ni mujarad wa ibadati kwa hivyo ni wajibu kuchunga kuhakikishwa thamani yake ya ki-roho tu bila kuangalia thamani nyenginezo.

Hizi ndizo thamani ya vitendo vyote, na ndizo mwanadamu hutenda ili kuzihakikisha katika kila kitendo katika vitendo vyake.

Na vipimo vya mujtama za ki-binadamu katika maisha yao ya duniani imma huwa mujibu wa thamani hizi. Na ikawa kadri inapo hakikisha mujtama thamani hizi na inavyodhamini kuhakikisha maisha mazuri na utulivu. Kwa hivyo ni juu ya Mwislamu kutia juhudi zake ili kuhakikisha thamani inayokusudiwa katika kila kitendo anachokitenda pindi anapokitenda kitendo hicho au kukiendelea mbio mpaka ashiriki katika maisha mazuri ya mujtama na kuinyanyua, na kudhamini kwa wakati huo huo maisha mazuri kwake yeye na utulivu.

Na thamani hizi hazitenganiki wala hakuna usawa katika dhati zake kwa sababu hakupatikani baina yake takhsisi yeyote ili ifanywe kuwa ni msingi wa kusawazisha kwa baadhi yake au kufadhilisha baadhi juu ya baadhi, bali ni natija aliokusudia mwanadamu pindi anapotenda kitendo kwa hivyo haimkiniki kuziweka katika mizani moja. Wala hazipimwi kwa kipimo kimoja kwa sababu hukhtalifiana ikiwa hazigongani. Isipokuwa mwanadamu ni katika hali yake kufadhilisha baina ya thamani ili achague lililo bora, hata kama si bora au sawa lakini mwanadamu haridhiki kwa hilo bali hufadhilisha na hufanya usawa baina yake. Na kufadhilisha huko na kufanya usawa haikujengwa juu ya nafsi ya thamani bali imejengwa juu ya yale yaliomsibu kutokamana nayo. Na juu ya hayo mwanadamu kwa nafsi yake amejenga kufadhilisha na usawa baina ya thamani. Na kwa kinachovuliwa kwake na thamani hizi katika manufaa au madhara, kwa hivyo hufanya nafsi yake kuwa ni kipimo au kufanya athari ambayo husibu dhati yake katika thamani hizi kuwa ni kipimo. Na huwa kwa hakika ni kufadhilisha baina ya

athari ya thamani kwa dhati yake kwa hivyo hukhtalifiana kufadhilisha kwao baina yake.

Watu ambao wameghilibiwa na hisia za kiroho na kumilikiwa na msukumo wake na wenye kupuuza thamani ya ki-mada, wao hufadhilisha thamani ya kiroho juu ya thamani ya ki-mada na huelekea kwa ibadati na kuupa nyongo mada. Kwa hivyo hutweza maisha kwa sababu maisha ni mada na husababisha kuregelea nyuma kwake ki-mada. Huporomoka kwa sababu yao mustawa (kiwango) cha mujtama wanaoishi ndani yake kwa kuenea ndani yake uvivu na ulegevu.

Na watu ambao wameghilibiwa na msukumo wa ki-mada na kumilikiwa na starehe na kupuuza thamani ya kiroho, wao hufadhilisha thamani ya ki-mada na huelekea kuihakikisha. Kwa hivyo huzidi kwao mwelekeo/thamani (*mathal*) ya juu na mujtama wanaoishi ndani yake huchanganyikiwa kwa sababu yao, na huenea ndani yake shari na ufisadi.

Kwa haya imekuwa ni makosa kumwacha mwanadamu kupima thamani hizi bali ni wajibu kupimwa na muumba wa mwanadamu naye ni Allah. Kwa hivyo imekuwa hapana budi awe mteremshaji Sheria (*Ash-Shari'*) ndiye anayempangia mwanadamu thamani hizi na kumpangia wakati wa kuzitenda, na kwa mujibu wake atazichukuwa mwanadamu.

Ameshabainisha *Ash-Shari'* suluhisho la matatizo maishani kwa maamrisho ya Allah na makatazo Yake, na akamlazimisha mwanadamu kupeleka maisha haya kwa mujibu wa maamrisho na makatazo hayo. Pia amebainisha vitendo ambavyo huhakikisha thamani ya kiroho nazo ni ibadati ambao alizoziwajibisha na kuzifanya sunna. Pia amebainisha sifa ambazo huhakikisha thamani ya ki-akhlaqi. Na akamwachia mwanadamu kuhakikisha thamani ya ki-mada ambazo humlazimu yeye ili akidhi dharura zake na mahitaji yake na yaliyo zaidi ya dharura na mahitaji kwa mujibu ya nidhamu maalumu aliyombainishia na kumwamrisha asende kinyume

nazo. Na hapana budi kwa Mwislamu ila kutenda kwa ajali ya kuhakikisha thamani hizo kwa mujibu ya maamrisho ya Allah na makatazo Yake na kipimo kwa kiwango alichokibainisha *Ash-Shari'*.

Kwa hivyo kuhakikishwa katika mujtama thamani kwa kiwango ambacho hulazimika nayo kama mujtama maalumu. Na hupima mujtama huu kwa vipimo vyake na juu ya msingi huu ni wajibu kutenda kwa ajili ya kuhakikisha thamani ili ipatikane mujtama wa Kiislamu kwa mujibu wa mtazamo wa Kiislamu maishani.

Na kwa hayo huwa kitendo cha mwanadamu ni mada anachokitenda mwanadamu kama mada isipokuwa yeye pindi anapokitenda hudiriki fungamano lake na Allah. Kwa hali ya kuwa kitendo ni halali au haramu, hukitenda au kujizuia kukitenda kwa msingi huu. Na huku kudiriki mwanadamu fungamano lake na Allah ndio roho, na ndio inayomlazimisha mwanadamu kujua Sheria ya Allah ili apimie vitendo vyake. Atafahamu kheri kutoka shari pindi anapojua yanayomridhisha Allah katika vitendo na yanayomkasirisha Allah na atatofautisha baya (*qabih*) kutoka zuri (*hasan*) pindi anapodomkezea *Ash-Shari'* kitendo kizuri na kitendo kibaya. Na kwa haya humkinika kwake yeye pindi anapotenda kitendo na akadiriki fungamano lake kwa Allah asongea mbele kutenda kitendo au kuepukana ndio kwa mujibu wa kudiriki huko kwa sababu yeye anajua aina ya kitendo na sifa yake na thamani yake. Na kufikia hapa imekuwa falsafa ya Kiislamu ya kuunganisha mada na roho yaani ni kufanya vitendo na venye kupelekwa kwa mujibu wa maamrisho ya Allah na makatazo Yake. Na imekuwa falsafa hii ni daima na lazima kwa kila kitendo jinsi kitakavyo kuwa kichache au kingi, kidogo au kikubwa. Na ikawa ndio mtazamo wa maisha, na ilipokuwa aqeeda ya Kiislamu ndio msingi wa maisha, na ndio msingi wa falsafa na msingi wa nidhamu, ilikuwa hadhara ya Kiislamu—ambayo ni mkusanyiko wa fahamu juu ya maisha kwa mtazamo wa Kiislamu—iliojengwa juu ya msingi mmoja wa kiroho nayo ni aqeeda. Na ikawa mtazamo wake kwa maisha ni kuunganisha mada na roho, na

ikawa maana ya kunali mafanikio (*sa'ada*) katika mtazamo wake ni radhi za Allah.

Inapokuwa aqqda ndio inaotatua tatizo kubwa nayo ndio msingi wa vitendo vya mwanadamu, na ndio inayosimama juu yake mtazamo wa ki-maisha, na falsafa ambayo hudhibiti vitendo hivyo basi nidhamu ambazo zilizotokamana na aqeeda ndio ambazo hutatua matatizo ya mwanadamu na kumpangia vitendo vyake kwa nidhamu kamili. Kwa hivyo imekuwa kutabikishwa kwake ni sehemu muhimu katika kupima hali ya serikali (*Dar*) kuwa serikali ya kikafiri ya serikali ya Kiislamu.

Serikali ambayo hutabikishwa ndani yake nidhamu za Kiislamu na kuhukumiwa ndani yake kwa yale aliyoyateremsha Allah, na huwa amani/usalama (*aman*) wake ni kwa amani ya Kiislamu huwa ni serikali ya Kiislamu (*Dar al-Islam*) hata kama wengi wa wakazi wake sio Waislamu. Na serikali isiokusanya ndani yake mambo haya miwili huwa ni serikali ya kikafiri (*Dar al-Kufr*) hata kama wengi wa wakazi wake ni Waislamu. Na kufikia hapa, la kutegemewa—baada aqeeda—ni juu ya nidhamu za Kiislamu na kwa kutabikishwa kwake katika kila nyanja ya maisha. Kwa sababu kutabikishwa kwa nidhamu hii pamoja na aqeeda hujenga katika Umma akili ya Kiislamu na hisia za Kiislamu, ujengaji wa ki-maumbile unaomfanya Mwislamu shaksiya wa hali ya juu wa kipekee.

Uislamu umekwisha mtazama mwanadamu kikamilifu bila kumgawanya vipande, na ukampangia vitendo vyake kwa hukmu za ki-Sheria mpango mmoja unaolingana, vyovyote yatakavyozidi na kutofautika vitendo hivi. Na hukmu hizi za ki-Sheria ndizo nidhamu za Kiislamu zinazotatua matatizo ya mwanadamu. Isipokuwa pindi zinapotatua matatizo yake huyatatua kwa hali ya kuwa kila tatizo lahitaji tatuo yaani kwa hali yake kama mas'ala yanayo hitajia hukmu ya ki-Sheria yaani hutatua matatizo yote kwa tatuo moja kwa sifa yake kama tatizo la ki-binadamu sio kwa sifa yeyote nyengine. Nayo pindi inapotatua tatizo la ki-uchumi mithali kama matumizi (*nafaqah*)

au tatizo la utawala kama kumtawaza Khalifa au tatizi la kijamii kama ndoa, hazitatui kwa sifa yake kuwa ni tatizo la ki-uchumi au kwa sifa yake kama tatizo la ki-utawala au tatizo la kijamii bali hulitatua kwa sifa yake kama matatizo ya ki-binadamu na hulivulia (*istinbat*) utatuzi yaani kwa hali yake kama mas'la yanayovuliwa kwake hukmu ya ki-Sheria. Uislamu una twarika moja ya kutatua matatizo ya mwanadamu nayo ni kufahamu tatizo linalo tukia na kuvua hukmu ya Allah juu yake kutokamana na dalili za ki-Sheria fafanuzi.

Na nidhamu za Kiislamu ni hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na ibadati, akhlaqi, vilaji, mavazi, maingiliano (*mu'malat*) na nidhamu za kuadhibu wahalifu.

Hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na ibadati, akhlaqi, vilaji na mavazi havina *'illa* (sababu yenyewe ya kuteremshwa hukmu). Asema (SAAW): "**Imeharamishwa tembo (*khamr*) kwa asili yake**." Amma hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na maingiliano na nidhamu za kuadhibu wahalifu, hizo zina *'illa* kwa sababu hukmu za ki-Sheria juu yake zimejengwa juu ya *'illa* liliosababisha kuwekwa hukmu kwa ajili yake. Hakika wamezowea wengi kuweka *'illa* ya ki-manufaa kwa ahkamu zote wakiathirika na fikra kiongozi wa ki-magharibi na hadhara ya ki-magharibi ambao hufanya manufaa pekee yake kuwa ni msingi wa vitendo vyote. Haya hugongana na fikra kiongozi ya Kiislamu unaofanya roho ndio msingi wa vitendo vyote, na kuunganishwa kwake na mada ndio inayodhibiti vitendo. Na kwa haya hakika wa hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na ibadati, akhlaqi, vilaji na mavazi hazina sababu kata kata kwa sababu hukmu hizi hazina *'illa* bali huchukuliwa tu kama zilivyopokewa na dalili wala hazijengwi kata kata juu ya *'illa*. Swala, saumu, hijja, zakaa, jinsi ya kuswali na idadi ya rakaa zake, amali za hijja, nisabu ya zaka na mithali yake huchukuliwa vile vile kama zilivyokuja, na hupokelewa kwa kukubaliwa na kusalimu amri bila ya kuangalia *'illa* yake bali hata haitafutwi *'illa* yake. Hivyo hivyo kuharamishwa kwa mfu, nyama ya nguruwe na yasiyokuwa hayo milele haitafutwi *'illa* yake bali ni

katika makosa na hatari kutafutwa *‘illa* kwa sababu lau ingelitafutwa *‘illa* za ahkamu za vitu hivi natija yake ni lau hino *‘illa* itapotea basi hukmu itapotea kwa sababu *‘illa* huzunguka na kile kinachofanyia kazi (*ma’lul*) kwa kuwepko na kutokuweko. Lau tutalazimisha kuwa *‘illa* ya udhu ni usafi na *‘illa* ya swala ni mazoezi na *‘illa* ya saumu ni afya…na mithali yake, natija yake itakuwa kwamba hali ikipotea *‘illa* basi hukmu haitokuwepo ilhali mambo si hivyo. Kwa hivyo imekuwa ni hatari kwa hukmu kutafutiwa *‘illa* ya kuitenda. Ni wajibu kuchukuliwa hukmu za ibadati kama zilivyo bila kuzitafutia *‘illa*. Amma kuhusu hekima, ni Allah pekee yake ndiye anayeijua na akili zetu haziwezi kudiriki uhakika wa dhati ya Allah basi hatuwezi kudiriki hekima yake. Amma hekima zilizopokewa kutokamana na dalili kama msemo Wake ta’ala:

**{ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنْ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ } (العنكبوت: 45**

“*Bila shaka swala hukanya mambo machafu na maovu*” [TMQ 29:45] na msemo Wake:

**{ لِيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ } (الحج: 28**

“*ili washuhudie manufaa yao*” [TMQ 22:28] na msemo Wake:

**{ وَمَا آتَيْتُمْ مِنْ زَكَاةٍ تُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ فَأُوْلَئِكَ هُمْ الْمُضْعِفُونَ } (الروم: 39**

“*na mnayoyatoa kwa ajili ya zakaa kwa kutaka radhi ya Allah, basi hao ndio wazidishao*” [TMQ 30:39]

Na hekima nyenginezo zilizotajwa waji na dalili, hizi zakoma juu ya dalili na huchukuliwa jinsi ilivyo wala haizidishiwi juu yake. Na isiyothubutu kwa dalili basi haitafutiwi hekima kama isivyotafutiwa *‘illa*.

Hii ni katika ibadati. Amma akhlaqi, hizo ni thamani iliojaaliwa ahkamu zilizo bainisha fadhila na akhlaqi njema na zilizo kinyume nazo, kama zilivyojaaliwa kuwa ni natija ya ibadati na yanayolazimika kuzingatiwa katika maingiliano. Hii ni kwa sababu Uislamu umelenga katika Sheria zake kumpeleka mwanadamu katika njia ya ukamilifu mpaka afikie katika daraja ya juu kabisa anayoiweza, na ina pupa asifike na sifa ya juu ya

pupa abakie akisifika nazo. Akhlaqi njema ni thamani zinazochungwa kutekelezwa pindi anaposifika nazo nayo huhusika na zile fadhila zilizotajwa wazi na Sheria, na huchungwa thamani yake pindi anapotenda fadhila hino na anaposifika nayo. Akhlaqi ni sehemu ya Sheria ya Kiislamu na ni sehemu ya maamrisho ya Allah na makatazo Yake ambayo hapana budi kuhakikishwa katika nafsi ya Mwislamu ili atimize amali zake na Uislamu na akamilishe kutenda kwake kwa mujibu ya maamrisho ya Allah na makatazo Yake.

Mwislamu hasifiki na sifa za ki-akhlaqi kwa dhati zake wala si kwa sababu ya manufaa yaliyomo ndani yake, bali husifika nazo tu kwa sababu Allah ameziamrisha si kwa sababu cha kitu chochote chengine. Hasifiki Mwislamu kwa ukweli kwa sababu ya dhati ya ukweli wala si kwa sababu ya manufaa yaliyomo ndani yake bali ni kwa sababu Sheria imemwamrisha nazo.

Amma kutosifika Mwislamu na akhlaqi kwa sababu ya dhati ya akhlaqi, hilo huregelea sifa ya vitenda. Huenda likawa kitendo ambacho amekitenda mwanadamu kwa dhati yake ni ki-ovu na yeye akidhania ni jema na akitende. Na huenda kuwa sifa ambayo amesifika nayo kwa dhati yake ni sifa ya uovu na yeye akidhania ni sifa njema na asifike nalo na wakati huo atukie katika kosa la kutenda mwanadamu kwa dhati ya akhlaqi. Na kisichodokezwa na Uislamu kuwa ni sifa njema na sifa mbaya na akazitenda mwanadamu kwa msingi wa ufafanuzi huu, haimkiniki kuwa kusifika kwake na sifa hizi imelingana na hukmu za ki-Sheria. Kwa hivyo haijuzu kwa Mwislamu kusifika na ukweli kwa dhati ya ukweli wala harehemu wanyonge kwa dhati ya huruma, wala hasifiki na akhlaqi kwa dhati ya akhlaqi bali husifika nazo kwa sababu Allah amemwamrisha nazo. Kwa sababu hakika za akhlqai hizi hutegemea juu ya aqeeda ya Kiislamu, na hichi ndicho kitu cha undani wake. Na hii ndio hutosheleza kumakinisha akhlaqi katika nafsi na kubakia kwake kuzisafisha kutoka kila uchafu, na kuiweka mbali na kila sababu za kuzifisidi. Kwa hivyo imekuwa kinga ya akhlaqi kwa nafsi ni

kujifunga na yaliyokuja ya dalili, na kufungika katika msingi wa kiroho na kujengwa juu ya aqeeda ya Kiislamu.

Amma kutosifika mwanadamu na akhlaqi kwa sababu ya yaliyomo ya manufaa ndani yake hilo huregelea kuwa manufaa sio linalokusudiwa katika akhlaqi wala haijuzu kuwa ndio iliokusudiwa ili isifisidike na ili isizunguke nayo popote inapozunguka. Akhlaqi ni safa ambazo hapana budi kwa mwanadamu kusifika nazo kwa utiifu na khiyari kwa msukumo wa uchaji Mungu. Na Mwislamu hatendi vitendo vya ki-akhlaqi kwa sababu hufaa au hudhuru maishani bali huvitenda kwa kuitikia maamrisho ya Allah na makatazo Yake, na hili ndilo linalofanya kusifika kwa akhlaqi njema ni lenye kudumu na thabiti isizunguke panapo zunguka manufaa.

Hizi akhlaqi zinazosimama juu ya kubadilishana manufaa humfanye mwenye kuzitenda kuwa ni munafiq. Huwa ndani yake sio dhahiri yake kwa sababu akhlaqi kwake imejengwa juu ya manufaa na huzunguka katika nafsi yake pale panapo zunguka manufaa kwa sababu mwanadamu huzungusha hukmu zenya *‘illa* juu ya *‘illa* zake wala haitakidi kuwepo kwake wala uwajibu wake pindi anapoona kuwa sababu yake imeondoka.

Kwa hivyo zimekuwa akhlaqi hazina *‘illa* wala haijuzu kuwekewa *‘illa* bali huchukuliwa kama Sheria ilivyokuja nazo bila kuangalia *‘illa* yeyote mwengine mwa *‘illa*. Ni katika makosa na hatari akhlaqi kuwekewa *‘illa* ili isibatilike kusifika nazo kwa kupotea *‘illa* yake.

Kufikia hapa hubainika kuwa makusudio ya ibadati ni thamani ya kiroho pake yake na makusudio ya akhlaqi ni thamani ya ki-akhlaqi peke yake, na ni wajibu kubakia kwa thamani hizo zilizokusudiwa sio nyengine. Haijuzu kubainisha yaliyomo katika ibadati na akhlaqi miongoni mwa faida na manufaa kwa sababu kubainisha hivi ni hatari kwake kwa kusababisha unafiqi katika wenye kuabudu na walio na akhlaqi, na hupeleka

kuwachwa kwa ibadati na akhlaqi pindi isipo dhihiri faida yake wala kuonyesha wazi manufaa yake.

Amma hukmu za ki-Sheria zinazoambatana na vitendo vya mwanadamu katika mafungamano yake pamoja na mwanadamu, miongoni mwa dalili zilizokuja nazo hukusanya *‘illa* kama msemo Wake ta’ala katika kuwapa ngawira (*fai*) ya Banu Nadhir kwa muhajirina bila ma-ansari:

{ كَيْ لاَ يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ } (الحشر: 7

"*ili isiwe kinyang’anyiro (mzunguko) baina ya matajiri wenu tu*" [TMQ 59:7] Na nyengine zisiokusanya *‘illa* kama msemo Wake ta’ala:

وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا (البقرة: 275

"*Allah amehalalisha biashara na ameharamisha riba*"[TMQ 2:275].

Yaliyokuja kutoka dalili katika hukmu zilizo na *‘illa* basi huwekewa *‘illa* na kufanya kipimo (*qiyas*) juu yake. Yaliyokuja kutoka dalili zisizokuwa na *‘illa* basi haziwekewi *‘illa* kata kata na kufuatilia hazifanyiwi *qiyas*. Na *‘illa* inayotambuliwa ni *‘illa* iliyowekwa na Sheria yaani iliyodokezwa na dalili ya ki-Sheria kutokamana na Kitabu na Sunna kwa sababu hizi mbili ndizo dalili za ki-Sheria peke yake. Kwa hivyo *‘illa* inayojengwa juu yake hukmu ya ki-Sheria iliyo na *‘illa* ni *‘illa* ya ki-Sheria wala sio *‘illa* ya ki-akili yaani ni wajibu iwe imekuja kwa dalili iliyo wazi (*sareeh*) au kwa kudokezwa (*dalalah*) au kwa kuvuliwa (*istinbat*) au kwa kupimwa (*qiyas*). *‘Illa* hino huzunguka pale inapozunguka kilichowekewa *‘illa* kwa kuwepo na kutokwepo basi hukmu huzunguka na *‘illa* yake pindi inapozunguka. Utaona kitu kimoja kinakatazwa katika hali (fulani) kwa sababu ya *‘illa* ya ki-Sheria, na pindi inapo ondoka *‘illa* hio hujuzu kitu hichi basi hukmu ya ki-Sheria huzunguka pamoja na *‘illa* inapokuwepo na kutokuwepo. Inapopatikana *‘illa* hupatikana hukmu na inapokosekana *‘illa* hukosekana hukmu.

Isipokuwa kuondoka hukmu kwa sababu ya kuondoka *‘illa* yake haimanishi kata kata kuwa hukmu imebadilika bali hukmu ya

ki-Sheria juu ya mas’ala ni hiyo hiyo haibadiliki. Bali hukmu huondoka tu pindi inapoondoka *‘illa* yake na hurudi hukmu kwa kurudi *‘illa* yake.

Na hali ya kuwa hukmu huzunguka pamoja na *‘illa* katika kuwepo kwake na kutokwepo kwake haimaanishi kuwa hukmu hio imebadilika kwa kubadilika zama na mahali kwa mwito wa kuwa kupata maslaha na kuepesha ufisadi (*jalab al-masalih wa dar’u al-mafasid*) ndio *‘illa* ya hukmu za ki-Sheria inayobadilika kwa kubadilika zama na mahali basi hubadilika hukmu kwa kubadilika kwake. Hilo ni kwa sababu kupata maslahi na kuepusha ufisadi sio *‘illa* kata kata ya hukmu za ki-Sheria kwa sababu haijakuja kudokeza kuwa kupata maslahi na kuepusha ufisadi ndio *‘illa* ya humu za ki-Sheria. Wala haijakuja dalili yeyote inayoidokeza kuwa ni *‘illa* ya hukmu maalumu basi haiwi ni *‘illa* ya ki-Sheria.

Kisha *‘illa* ya ki-Sheria ni ile tu iliyodokewa na dalili ya ki-Shera basi hapana budi kujifunga nayo na kusimama kwa maana yake, nayo haidokezi kuwa kupata maslahi na kuepusha ufisadi. Basi huwa *‘illa* ya ki-Sheria ni ile iliyokuja nayo sio kupata maslahi na kuepusha ufisadi. Na hino iliyokuja nayo dalili haikudokeza juu ya zama na mahali, wala haidokezwi na kitendo, bali imedokezwa na dalili ya ki-Sheria katika kubainisha *‘illa* ya hukmu, na dalili hino kata kata haibadilishwi basi hakuna thamani kwa zama na mahali hapa kama hakuna thamani ya kupata maslahi na kuepusha ufisadi.

Kwa hivyo, hukmu za ki-Sheria hazibadiliki kwa kubadilika zama na mahali bali hukmu ya ki-Sheria ni ile ile haibadiliki vyovyote itakavyo badilika zama na mahali.

Amma kubadilika desturi na ada za watu, hilo haliathiri katika kubadilisha hukmu kwa sababu desturi sio *‘illa* ya hukmu wala si msingi wake. Desturi imma imekhalifu Sheria au haikuikhalifu. Ikiwa imekhalifu Sheria basi Sheria imekuja kuifuta na kubadilisha kwa sababu miongoni mwa kazi za

Sheria ni kubadilisha desturi na ada mbovu kwa sababu ndio inayosababisha kuharibika kwa mujtama. Kwa hivyo haichukuliwi kuwa ni msingi wa hukmu ya ki-Sheria wala sio *'illa* yake, na haibadiliki hukmu kwa ajili yake. Na ikiwa haikhalifu Sheria, hukmu huthibitika kwa daili yake na *'illa* yake ya ki-Sheria sio kwa desturi hini hata kama haikhalifu Sheria. Kwa hayo ada haihukumu juu ya Sheria bali Sheria huhukumu juu ya ada na desturi. Basi hukmu za ki-Sheria dalili yake ni msemo/dalili (*nass*) na zina *'illa* ya ki-Sheria, na desturi na ada sio katika hizo kata kata.

Amma kuhusu kufaa kwa Sheria ya Kiislamu kwa kila zama na mahali, hilo hutokamana na upande wa kuwa Sheria ya Kiislamu hutatua matatizo ya mwanadamu katika kila zama na mahali kwa hukmu zake, na ni pana kwa kutatua matatizo yote ya mwanadamu jinsi zitakavyo kuwa mpya na kutofautika kwa sababu Sheria pindi inapotatua matatizo ya mwanadamu hutatua kwa sifa yake kama mwanadamu.

Na mwanadamu katika kila zama na mahali ni mwanadamu katika ghariza zake na mahitaji yake ya kiviungo wala habadiliki milele. Hivyo hivyo hukmu za kuzitatua hazibadiliki; kinachobadilika ni muundo wa maisha ya mwanadamu na hili haliathiri katika mtazamo wake maishani. Amma yanayokuwa mpya katika matakwa tofauti tofauti ya mwanadamu, hilo hutokamana na ghariza hizo na mahitaji ya kiviungo, na imekuja Sheria iliyo pana kutatua matakwo hayo yaliyo mpya na yanayotofautika jinsi yatakavyo badilika na jinsi yatakavyo badilika muundo wake. Na hilo limekuwa sababu miongoni mwa sababu zilizoikuza fiqhi. Isipokuwa upana huo katika Sheria haimaanishi kuwa ni 'kupanuliwa (Sheria)' kwa hali yakuwa inatabikishwa juu ya kila kitu hata kama inagongana nayo. Wala haimaanishi kuwa ni yenye kubadilika kwa hali ambayo hubadilika pamoja na zama bali humaanisha upana wa dalili ili kuvua (*istinbat*) hukmu tofauti tofauti na humaanisha upana wa hukmu ili kutabikishwa juu ya mas'ala mengi. Mfano husema Allah ta'ala:

{ فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ }(الطلاق: 6
"*Na kama watawanyonyeshea, basi wapeni ujira wao*"[TMQ 65:6].

Hakika aya hii huvuliwa kutokamana nayo hukmu ya ki-Sheria nayo ni mwanamke aliyepewa talaqa astahiki ujira wa kunyonyesha na huvuliwa kutokamana nayo pia hukmu ya ki-Sheria kuwa yeyote aliyeajiriwa anastahiki ujira anapofanya kazi yake sawa sawa awe aliojiriwa na mtu binafsi au alioajiriwa na watu jumla (*ajeer 'amm*). Hukmu hii hutabishwa juu ya mas'ala mengi miongoni mwake mfanyi kazi wa serikali, mfanyi kazi katika kiwanda, mkulima katika shamba na wanaofanana nao hustahiki kila mmoja wao ujira wake anapomaliza kazi yake kwa sababu yeye ni mwajiri binafsi (*ajeer khas*). Na seremala ambaye hutengeneza kabati, mshonaji ambaye hushona nguo na mtengeneza viatu anayetengeneza viatu na mifano yao hustahiki kila mmoja wao ujira wake anapotenda kazi yake kwa sababu yeye ni mwajiri jumla (*ajeer 'amm*). Na kwa kuwa kuajiriwa ni mkataba baina ya mwenye kuajiri na alioajiriwa, haingii ndani yake mtawala kwa sababu yeye hakajiriwa na Ummah bali yeye ni mwenye kutekeleza hukmu za ki-Sheria yaani mwenye kutabiksha Uislamu. Kwa hivyo hastahiki Khalifa ujira kwa kutenda kazi yake kwa sababu yeye amepewa bay'a ili azitekeleze Sheria na kubeba ulinganizi wa Kiislamu naye hakuajiriwa na Ummah. Hivyo hivyo wasaidizi (*mu'awin*) wake ambao ni viungo katika idara ya utendaji na ma-wali hawastahiki ujira kwa kutenda kazi zao kwa sababu kazi zao ni hukmu na wao sio waajiriwa. Kwa hivyo hawachukuwi ujira bali hukadiriwa makadairio yatakayo tosheleza mahitaji yao kwa sababu ya kushughulishwa kutotekeleza mambo yao khasa.

Upana huu wa dalili wa kuvua hukmu nyingi na upana wa hukmu unaotabikishwa juu ya mas'ala mengi ndio ambao unaofanya Sheria ya Kiislamu kutosheleza katika kutatua matatizo yote ya maisha katika zama zote na mahala na kila Umma na karne, wala sio kupanuliwa wala kubadilika.

Na dalili ya hukmu za ki-Sheria kutoka dalili (*nass*) ya Kitabu na Sunna hutatua matatizo yaliyosimama kwa sababu mteremshaji Sheria (*Ash-Shari'*) amekusudia kufuatwa maana sio kusimama juu ya dalili kwa hivyo huchunga katika kuvua hukmu upande wa *'illa* katika dalili pindi inapovuliwa hukmu kwa upande wa ki-Sheria.

Na dalili imma ime imejumulisha *'illa* ya hukmu au ichukuliwe *'illa* kutoka dalili nyengine au kutokomana na mjumuiko wa dalili. Na hata kama imevuliwa kutokamana na dalili yake lakini huchungwa ndani yake upande wa *'illa* wala haifungwi na sura iliokuja katika dalili iliokuja kutatua matatizo ambayo yaliyopo. Mfano wa hilo ni msemo Wake ta'ala:

**{ وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ } (الأنفال: 60)**

"*Waandalie nguvu mnazoziweza na farasi waliofungwa ili muwatishe kwazo (nguzu hizo) maadui wa Allah na adui wenu*" [TMQ 8:60].

Hukmu ni kuandaa nguvu na miongoni mwake ni vipando vya farasi. Na upande wa *'illa* katika hukmu ni kutishia adu. Pindi inapovuliwa leo kutoka dalili hukmu ya uandazi, tutachunga upande wa *'illa* katika hukmu na tutaandaa yale yatakayo hakikisha utisho kwa adui. Wala hatufungwi na yaliyotatuliwa nayo tatizo ambalo ilikwepo kwa yale yaliyopatikana katika dalili wa vipando wa farasi.

Hivi ndivyo inavyotendwa kutoka kila dalili inayovuliwa kutokamana nayo hukmu kwa sababu muradi wake ni kuhakikishwa upande wa *'illa* katika hukmu. Kwa hayo Sheria ya Kiislamu imeweka katika hukmu zinazoambatana baina watu katika maingiliano kwamba zijengwe juu ya *'illa*, na kuchungua katika dalili wakati wa kuvua hukmu kutokamana nayo upande wa uteremshaji Sheria (*tashri'*) sio sura iliyopokelewa katika dalili.

Kama inavyokuwa dalili ya Kitabu na Sunna ni dalili ya ki-Sheria juu ya hukmu, hivyo hivyo ijma ya masahaba (*Ijma as-Sahabah*) na *qiyas* huhisabiwa miongoni mwa dalili za ki-Sheria. Kwa hayo dalili za ki-Sheria za kijumla kwa hukmu za ki-Sheria ni Kitabu, Sunna, *Ijma as-Sahabah* na *qiyas*. Amma *madhab* ya sahaba mmoja katika mas'ala ya ki-ijtihadi, haiwi ni dalili ya ki-Sheria kawa sababu sabaha ni miongoni mwa watu wa ijtihadi na kukosa ni uwezekano kwake yeye. Na kwa kuwa masahaba wamekhtalifiana katika masa'la na akaenda kila mmoja wao kinyume na *madhab* ya mwengine, na lau ingefanywa *madhab* ya sahaba mmoja kuwa ni hoja zingekuwa hoja za Allah ni zenye kukhtalifiana na kugongana. Kwa hivyo haihisabiwi *madhab* ya sahaba kuwa ni dalili ya ki-Sheria bali hujuzu kuchukua kutoka kwake kama nyenginezo za *madhahib* yanayotambuliwa. Amma waliowafikiana juu yake masahaba katika hukmu, hino ni *madhab* kwao wao bali huwa ni ijma.

Amma Sheria ya watu kabla yetu, haihisabiwi kuwa ni Sheria kwetu sisi kwetu sisi wala haihisabiwi miongoni mwa dalili za ki-Sheria. Hata kama aqeeda ya Kiislamu yawajibisha imani kwa Mitume (*anbiyaa*) na Wajumbe (*rusul*) wote na kwa vitabu ambavyo vimewashuka, lakini maana ya imani kwao wao ni kusadikisha kwa utumwa wao na ujumbe wao na kwa yaliyo washukia katika vitabu, wala sio maana ya imani kwao wao ni kuwafuata kwa sababu baada ya kutumilizwa Muhammad (saw) wamekuwa watu wote ni wenye kuulizwa kuwacha dini zao na kufuata Uislamu kwa sababu haihisabiwi dini yeyote isiyokuwa dini ya Uislamu. Asema ta'ala:

**{ إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الإِسْلاَمُ } (آل عمران: 19**

"*Hakika dini mbele ya Allah ni Uislamu*" [TMQ 3:19] na asema ta'ala:

**{ وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الإِسْلاَمِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الآخِرَةِ مِنْ الْخَاسِرِينَ } (آل عمران: 85**

"*Anayetaka dini isiyokuwa ya Uislamu basi kattu haitakubaliwa kwake.Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara!*" [TMQ 3:85] Na hili ni wazi.

Na imevuliwa kutokamana nayo *qaida*: ‘Sheria ya watu kabla yetu sio Sheria kwetu.’ Na dalili juu ya hiyo ni kuwa masahaba wamewafikiana kuwa Sheria iliyomshukia Muhammad (SAAW) imezifuta Sheria zote zilizotangulia kwa sababu Allah ta’ala asema:

**{ وَأَنزَلْنَـا إِلَيْـكَ الْكِتَـابَ بِـالْحَقِّ مُصَـدِّقًا لِمَـا بَـيْنَ يَدَيْـهِ مِـنْ الْكِتَـابِ وَمُهَيْمِنًـا عَلَيْـهِ } (المائدة: 48)**

“*Tumekuteremshia Kitabu kwa haki kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvitawala*” [TMQ 5:48] yaani yenye kutawala na iliyo juu.

Na hukmu ya Qur’ani juu ya vitabu vilivyo tangulia ni kuzifuta Sheria zilizotangulia yaani imekuja kusadikisha na kuzifuta. Na imepokewa kutoka Mtume (SAAW) kuwa amemuona Umar bin Al-Khattab akiwa na kipande cha Taurati akiitizama basi akakasirika na akasema: “**Je, sikuja na yaliyo nyeupe na safi? Na lau angelikutana na mimi ndugu yangu Musa asingekuwa na khiyari ila kunifauta mimi**.” Pamoja na kuwa amali za hijja kama tawaf pambizoni mwa Ka’aba, kugusa jiwe jeusi na kuubusu na kufanya *say* baina Safa na Marwa zilikuweko katika zama za ujahiliyya, pindi sisi tunapozitenda na kuabudu nazo hatuzitenda kama amali ya Sheria zilizotangulia bali twazitenda tukizihisabu kuwa ni Sheria ya Kiislamu kwa sababu Uislamu imekuja nazo kama hukmu za ki-Sheria mpya wala sio kukiri Sheria zilizotangulia. Hivyo hivyo yote yaliyokuja kutoka dini zote zilizotangulia, hatuzitekelezi katuu; bali twatekeleza iliokuja nayo Sheria ya Kiislamu tu. Kwa hivyo huwa mnasara na myahudi ni wenye kukhutubiwa na Sheria ya Kiislamu na ni wenye kuamrishwa kuwacha Sheria zao kwa sababu Uislamu umefuta Sheria zao. Na ikiwa hilo ni wajibu kwa wafuasi wa Sheria ya ki-yahudi nawo ni mayahudi na manasara, basi vipi huombwa Mwislamu kuchukuwa Sheria ya wale kabla yake kuwa ni Sheria yake? Amma msemo wa Allah ta’ala:

**{ إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ }(النساء: 163**

“*Tumeketeremshia wahyi kama tulivyowafunulia Nuhu*” [TMQ 4:163],

Muradi wake ni kuwa ameteremshiwa wahyi kwake kama walivyo teremshiwa wahyi kwa wengineo miongoni mwa Mitume. Na msemo Wake ta’ala:

**{ شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا } (الشورى: 13**

“*Amewapa Sheria ya dini yale aliyomuusia Nuhu*” [TMQ 42:13]

Maana yake kupewa Sheria ya asli ya tawhid nayo ndiyo aliousiwa nayo Nuhu.Na msemo Wake ta’ala:

**{ ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا }(النحل: 123**

“*Kisha tukakufunulia ufuate milla ya Ibrahimu*” [TMQ 16:123]

Maana yake kufuata asli ya tawhid kwa sababu ‘*milla*’ maana yake ni asli ya tawhid. Na muradi wa aya hizi zote na zilizofanana nazo ni mbayana kuwa yeye (SAAW) sio mzushi katika utume bali ametumwa kama walivyotumwa wengineo, na kuwa asli ya tawhid ndio dini na ndio walioshirikiana nayo Mitume na Wajumbe wote. Amma yasiokuwa hilo kila Mjumbe ametumwa na dini. Asema ta’ala:

**{ لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا } (المائدة: 48**

“*Na kila katika nyinyi tumewajaalia Sheria na njia*”[TMQ 5:48].

Kwa hilo, hakika Sheria ya wale kabla yetu sio Sheria kwetu wala haihisabiwi miongoni mwa dalili za ki-Sheria ambao huvuliwa kutokamana nayo hukmu.

Asli katika kuvua hukmu ni kwa mujtahidina kwa sababu ujuzi wa hukmu ya Allah katika mas’ala haiwi ila kwa ijtihadi; kwa hivyo hapana budi ila kwa ijtihadi. Na wamesema wanavyuoni wa misingi (*usul*) kuwa ijtihadi ni faradhi ya kutosheleza (*fard kifaya*) juu ya Waislamu na haijuzu kwa zama miongoni mwa zam kukosekana mujtahid. Na ikiwa wote wamewafikiana kwa kuwacha ijtihadi ni dhambi, na hilo ni kwa sababu njia ya kujua hukmu za ki-Sheria ni kupitia ijtihadi. Na lau ingekosekana

zama kwa mujtahid anayemkinika kutegemewa katika kujua hukmu, hupelekea hilo kwa kutotendwa na kuzifuta hukmu na hilo halijuzu. Isipokuwa ijtihadi ina shuruti zake zilizofafanuliwa na ma-ulama wa *usul* na yahitaji mtazamo uliopana, ufahamu wa sahihi kwa dalili (*nusus*) na ujuzi kamili kwa lugha ya kiarabu. Na huhitajia fiqhi juu ya mas’ala ya ki-Sheria na kusimama juu ya dalili zake.

Kwa hivyo kuchukua hukmu bila mazingatio wala mtazamo mzuri haitwi kuvua (*istinbat*), kama haitwi mujarad ya kudhihiri maslahi katika hukmu kisha kufanya ujanja juu ya dalili na kuzibebesha yasiyokusudiwa nayo ili kustanbiti hukmu hino kuwa ni ijtihadi. Bali hilo ni kukosea dini ya Allah inayostahiki alieitenda adhabu kutoka kwa Allah.

Ndio mlango wa ijtihadi uko wazi lakini yako wazi kwa ma-ulama sio kwa wajinga. Mujtahidina ni aina tatu: Mujtahid *mutlaq*, mujtahid *madhab* na aina hizi mbili wana shuruti maalumu. Amma watatu, huyu ni mujtahid wa suala moja, naye ni mwenye uweza kufahamu dalili na kulifuata suala moja na dalili zake na dalili ya mujtahidina juu yake. Nayo ni lazima kwa kila Mwislamu anayetaka kujua hukmu ya Allah. Hakika Sheria imefanya asli ya kila Mwislamu achukuwe hukmu kwa nafsi yake kutokamana na dalili yaani awe mujtahid katika dini katika mas’ala ambao humlazimu.

Lakini baada ya kusajiliwa *madhahib* ya mujtahidina na kumakinishwa nguzo (*qawa’id*) za hukmu, fikra ya ijtihadi ilidhoofika katika miyoyo na mujtahidina wakawa wachache. Ikazidi kwa Waislamu wengi *taqleed* na ikawa ijtihadi nadra kwa Waislamu, mpaka ikavuka mipaka fikra ya *taqleed* mpaka wakatokea wenye kusema kufungwe mlango wa ijtihadi na uwajibu wa *taqleed*. Kwa ajili hayo watu wengi miongoni mwa Waislamu kama si wote wakawa *muqallideen*.

Na muqalidina ni vigawanyo viwili: *mutabi’* na *‘ammi*. Tofauti baina ya *mutabi’* na *‘ammi* ni kuwa *mutabi’* huchukuwa hukmu

ambayo amevua mujtahid mmoja baada ya kukinaika kwake kwa dalili ambayo ameitegemea wala hamfuata bila kuijua dalili yake. Na *'ammi* yenye ni mwenye kumfuata mujtahid katika hukmu za ki-Sheria bila ya kuchunguza dalili. Na *mutabi'* ni hali bora kuliko *'ammi*, na walikuwa wengi katika waliotangulia katika *mutabi'* kwa kujali kwao dalili. Ilipokuja zama za mporomoko na ikawa ngumu kwa watu kufuata (*itiba'*), wakawa wakifanya *taqlid* kwa ma-imamu na mujtahidina kwa hukmu bila ya kuchunguza dalili, na iliwashajiisha wao kwa hilo kunyamaza kwa ma-ulama na kuridhio kwao watu kuwa *'ammi* hata kama ni katika wenye kusoma. Na sababu ya kunyamaza ma-ulama juu ya hilo ni kuwa *taqleed* kwa asli yake yajuzu sawa sawa akiwa *muqallid* ni *mutabi'* au *'ammi*, isipokuwa asli kwa Mwislamu ni kuchukua hukmu kutokamana na dalili yake lakini yajuzu kwakwe yeye kuwa *muqallid* na yajuzu kwake yeye kuwa *mutabi'* yaani kujua hukmu na kujua dalili yake na kukinaika nayo. Na hino ndio inayomfanya Mwislamu awe mtu wa ijtihad hata kama kwa suala moja, na hii hutulazimu sisi katika zama zetu hizi. Na fatwa sio katika mlango wa ijtihadi katika suala moja kwa sababu haliingii katika ijtihadi bali ni aina duni zaidi wa utungaji katika fiqhi. Hilo ni kuwa limetokea baada ya zama za mujtahidina na zama za wanafunzi wao na wanafunzi wa wanafunzi wao. Hawa wakaelekea katika kusherehesha rai za *madhab* na kubainisha msingi wake na kuzimakinisha rai zake, na huhisabiwa zama hino kuwa ni zama la waridi kwa fiqhi. Zilitungwa katika zama hino vitabu mama vya fiqhi katika *madhahib* tofauti na ndizo zinazohisabiwa kuwa ni maregeo kwa mas'ala ya ki-fiqhi. Hayo yakaendelea mpaka karne ya saba hijri, kisha ikaja baada yake zama za mporomoko wa ki-fiqhi nao ni zama wa kusherehesha na ufafanuzi. Na nyingi wa zama hizi zilikuwa tupu kwa uvumbuzi, *istinbati* na ijtihadi hata katika suala moja. Kisha ikaja baada yake zama za mporomoko zaidi, wakaja katika zama hizo ma-ulama walioingilia katika taja mas'ala na hukmu bila kulenga sura zake na vitagaa vyake, na zikaitwa mas'ala hayo kuwa ni fatwa. Kwa hivyo hazisihi kuchukuliwa kuwa ni maregeo kwa hukmu, kama haisihi kuchukuliwa fatwa hizi kuwa maregeo ya hukmu za ki-

Sheria kwa kuwepo kwao mbali na njia ya ijtihadi katika kustanbiti hukmu.

Hivyo hivyo haijuzu kuchukuliwa kama maregeo ya hukmu za ki-Sheria zile maregeo zilizotungwa kwa njia ya kuweka Sheria ki-kanuni (*taqneen tashri'ii*) kwa sababu ni dhihirisho miongoni mwa madhihirisho wa *taqleed* kwa kanuni za ki-magharibi. Na kwa kuwa kuwekwa kanuni hizi hupelekwa na njia ya kufupisha fiqhi na huzidiwa na kuchukuliwa mas'ala ya ki-fiqhi yasiyo na dalili au dalili zake ni dhaifu. Na pia kuzidiwa na roho ya kutembea na zama na taawili ili iwafikiane na mtazamo wa ki-magharibi katika kutatua matatizo pamoja na kukosekana upande wa uwekaji Sheria (*tashri'*) na kukosekana ndani yake ijtihadi. Basi hazifai kutabikishwa na pia hazifai kufanywa maregeo, na kuwepo kwake imekuwa ni balaa kwa fiqhi na uwekaji Sheria kwa sababu ilikuwa ni majaribio ya ki-*taqleed* uliodhoofisha ujuzi wa watu kwa fiqhi ya Kiislamu pamoja na kuwa utajiri uliopo katika fiqhi ya Kiislamu ni mwingi sana nao ni tajiri mkubwa wa ki-fiqhi katika umma zote. Na ni dharura kwa ma-kadhi na viongozi, lakini umewekwa kwa njia ya ki-*taqleed* juu ya sura ya ki-kanuni wakaifupisha na kuiharibu. Ikawafanya ma-kadhi kuwa ni wajinga katika fiqhi pindi walipo jitosheleza na ujuzi wa kanuni hizi. Isitoshe, ilikuwa imepoteza muundo wa ki-kanuni kwa sababu ilikuwa ni maelezo ya mkusanyiko wa dalili (*nusus*) wa ki-fiqhi za baadhi ya ma-*fuqaha* iliopokelewa kwa idadi (*arqam*) zinazofuatana. Wala haikujaribiwa ndani yake kuweka qai'da jumla ambao itakuwa ni maudhui ya mada na mas'ala kuwa chini yake, bali imezifanya mas'ala yenyewe kuwa ndio ni mada na hii ndio isiowafikiana pamoja na utangaji wa ki-kanuni mpaka yale yaliokuja katika baadhi ya mada katika qaida zimekuja kwa qaida zisizokuwa za ki-jumla na hazikuwa ila ni maarifa yaliyonukuliwa kutoka vitabu vya fiqhi, na imekurubia kuwa zote ni katika jinsi hii. Kwa hayo haijuzu kuchukuliwa kanuni hizi wala kuchukuliwa kama maregeo kwa sababu ya kufisidika mbinu zake, uchache wa maalumuti zake na umbali wake na

hukmu za ki-Sheria zinazotambuliwa zilizotegemea dalili fafanuzi.

Na kuweka katiba na kanuni ili kudhamini fiqhi ya ma-kadhi ya viongozi, ni lazima ipitie njia za kuweka Sheria zifuatazo:-

1. Ni lazima isomwe matatizo ya mwanadamu na kuweka katiba jumla itakayo kuwa kwa umbo la qaida mkusanyiko (*kuliyya*) zilizo jumla au hukmu za ki-Sheria za kijumla na ziwe zimetegemea fiqhi ya Kiislamu. Na ni lazima zichukuliwe imma kutokamana na rai ya mujtahid katika mujtahidina pamoja na kujua dalili yake na kukinaika nayo, au imma kutokamana na Kitabu na Sunna au ijma ya masahaba au *qiyas* lakini kwa ijtihadi ya ki-Sheria hata kama ni ijtihadi ya kivipande nayo ni ijtihadi juu ya suala moja. Na ni lazima idokezwe sababu zilizowajibisha katika kila kifungu katika *madhab* ambao ameitegemea na dalili yake au kwa dalili ambayo amestanbiti kutokamana nayo. Wala kattu asizingatie hali mbaya ilioko mbele ya Waislamu wala hali ya umma nyenginezo wala nidhamu zisiokuwa za Kiislamu.

2. Na ziwekwe hukmu za ki-Sheria (*mashari'*) kwa kanuni za kuadhibu, haki, ushahidi na nyenginezo juu ya msingi uliotangulia ikiambatana na katiba pamoja na kuashiriwa kwa madhab na dalili, na iwe na matamshi ya ki-kanuni kwa misingi jumla ili iwe ni maregeo ya ki-fiqhi kwa ma-kadhi na watawala.

3.Na ziwe dalili (*nusus*) za ki-Sheria, fiqhi ya Kiislamu na elimu ya usul-ul-fiqhi ndio maregeo katika kufasiri katiba na kanuni kwa ma-kadhi na watawala mpaka tuwasahilishie mbinu za ufahamu wa ki-ndani.

Na haifai kwa kadhi kuhukumu kwa yale yaliokhalifu yaliyotabanniwa na serikali katika hukmu za ki-Sheria kwa sababu: "Amri ya Imamu hutekelezwa kwa dhahiri na batini". Amma kwa yale yaliyomfikia na yeye katika ma-kesi juu ya yasio-tabanniwa ki-hukmu na serikali, kadhi atahukumu kwa

hukmu ya ki-Sheria anayoiona yeye kuwa inaambatana na suala sawa sawa iwe ni rai ya mujtahid miongoni mwa mujtahidina au ni rai alistanbiti mwenyewe kwa ijtihadi yake.

4. Na itiwe maanani pindi zinapostanbitiwa hukmu na pindi zinapotabanniwa ufahamu wa *waqi'ah* na kufahamu uwajibu katika kutatua tukio (*waqi'ah*) na dalili ya ki-Sheria nayo ni kufahamu hukmu ya Allah ambayo amehukumu nayo katika tukio (*waqi'ah*) hino kisha hutabakishiwa moja wapo juu ya nyengine. Na kwa maana nyengine ni kuunganisha ujuzi juu ya waquah na kuifahamu pamoja na kujua hukmu ya Allah.

Na hutekeleza serikali Sheria ya Kiislamu juu ya kila mwenye kubeba uraia wake sawa sawa awe ni Mwislamu au asie Mwislamu. Amma wasiokuwa Waislamu huwachwa na wanyoitakidi na wanyoyaabudu na huamiliwa katika mambo ya vilaji na vinywaji na mavazi kwa mujibu wa dini zao ndani ya nidhamu jumla na huamuliwa mambo yao ya ki-binafsi baina yao kama kwa mfano ndoa na talaqa kwa mujibu wa dini zao. Amma yaliobakia katika mambo ya Sheria ya Kiislamu miongoni mwa maingiliano (*mu' amalat*), nidhamu za kuadhibu wahalifu, nidhamu za hukmu, uchumi na nyenginezo hizo hutekelezwa juu ya wote na huko kutekelezwa kwake sawa sawa ni juu ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Amma Waislamu, serikali hutekeleza juu yao Sheria yote ya Kiislamu kutoka ibadati, akhlaqi, maingiliano, nidhamu ya kuadhibu wahalifu (mpaka mwisho). Na wajibu wa serikali ni kutabikisha Uislamu kikamilifu na kuchukulia kutabikishwa kwake juu ya wasiokuwa Waislamu kama ulinganizi kwao kwa Uislamu. Kwa sababu Sheria ni jumla kwa wanadamu wote na huitabikisha serikali katika biladi yeyote inayoitawala kwa kubeba ulinganizi kwao kwa sababu siri ya ukombozi wa Kiislamu huwa ni kubeba ulinganizi wa Kiislamu.

Uislamu ina aqeeda inayotakomana kwayo nidhamu, na nidhamu hii ni hukmu za ki-Sheria zilizostanbitiwa kutokana na dalili fafanuzi na imebainisha Uislamu katika nidhamu jinsi

ambavyo itakayotekelezwa hukmu zake kwa hukmu za ki-Sheria. Na hukmu hizi za ki-Sheria ambazo hubainisha jinsi ya kutekeleza ndio twarika (*tariqa*) na zisizokuwa hizo huwa ni fikra na kufikia hapa huwa Uislamu ni fikra na twarika. Aqeeda na hukmu za ki-Sheria ambazo hutatua matatizo ya mwanadamu ndio fikra na hukmu za ki-Sheria ambazo hubainisha jinsi ya kutekeleza utatuzi huu, kuhifadhi aqeeda na kubeba ulinganizi ni twarika. Na kwa haya imekuwa twarika ya Kiislamu ni katika jinsi ya fikra yake na ni sehemu yake, basi haijuzu kubakia ulinganizi kwa Uislamu juu ya kubainisha fikra yake bali ni wajibu ikusanye pia twarika. Na kwa hayo umekuwa mfumo ni mkusanyiko wa fikra na twarika. Na imani juu ya twarika ni kama imani juu ya fikra basi imekuwa lazima iwe twarika pamoja na fikra kikamilifu bila ya kutenganishwa; na ifungwe pamoja fungamano madhubuti kiasi ambacho haitumiwi kutabikishwa fikra ya Kiislamu ila kwa twarika ya Kiislamu na huwa mkusanyiko wake ndio Uislamu ambao ndio inayo hukumiwa na hubebwa ulinganizi kwayo. Na maadamu twarika ipo katika Sheria basi ni wajibu ifungwe ndani yake na yaliyothubutu ki-Sheria na yaliyostanbitiwa kutokamana na dalili zake. Kama ilovyo thubutu katika Kitabu na Sunna hukmu za fikra hivyo hivyo ilithubutu ndani yake hukmu za twarika. Msemo Wake ta'ala:

**{ وَإِمَّا تَخَافَنَّ مِنْ قَوْمٍ خِيَانَةً فَانْبِذْ إِلَيْهِمْ عَلَى سَوَاءٍ } (الأنفال: 58**

"*Na ikiwa mwaogopa khiyana kutoka watu, itupe kwao kwa usawa*" [TMQ 8:58]

Ni katika hukmu za twarika na hivyo hivyo msemo wake (SAAW): "**Msitamani kukutana/kupambana na maadui na mnapo kutana/kupambana nao subirini**" ni katika hukmu za twarika**.** Na hivyo hivyo hukmu zilizosalia za twarika hustanbitiwa kwa ijtihadi kutokamana na Kitabu, Sunna, Ijma as-Sahaba na Qiyas kama hukmu zilizosalia. Na ilipokuwa Sunna ndio yenye kuibainisha Kitabu imekuwa fikra ni ya kijumla katika Kitabu ikifafanuliwa katika Sunna. Na imekuwa twarika hivyo hivyo ni ya ki-jumla katika Qur'an iliyo fafanuliwa katika Sunna. Kwa hivyo imekuwa lazima kwetu

kujaalia taa (*nibras*) ya uongofu ni bwana wetu Muhammad Mtume wa Allah na tuchukue hukmu za twarika kutokamana na vitendo vyake vinavyopatikana katika Sera yake, maneno yake na kunyamaza kwake kama tunavyo chukua kutokamana na Qur'ani kwa sababu yote hayo ni Sheria. Na tujaalie kigizo chetu katika kufahamu ni Sera ya ma-khalifa walioongoka na masahaba waliosalia kama twafanya akili zetu ni chombo cha kivitendo (*fi'ala*) kufahamu na kustanbiti kwa mujibu wa mwelekeo wa ki-Sheria.

Na hukmu za ki-Sheria ambazo hubainisha jinsi ya utendaji hudokeza kwa vitendo basi hapana budi kutenda vitendo hivyo sawa sawa ziwe miongoni mwake zinazoambatana na utabikishaji au zinazoambatana na ubebaji wa da'wa. Na vitendo hivyo sio vyombo kwa sababu chombo (*wasila*) ni kifaa kinachotumika wakati wa kutenda kitendo, na hutofautishwa kwa kutofautika vitendo, hubadilika kwa mujibu ya dhurufu na huamuliwa na aina ya kitendo. Kwa hivyo hailazimiki ndani yake hali maalumu. Amma vitendo ambavyo hudokezwa na twarika hivyo havibadiliki bali hutendwa kwa mujibu ya maana ya dalili wala haijuzu kutenda kitendo tofauti na kilichobainishwa na Sheria. Na wala hakitendwi kitendo nje ya pahala pake iliobainishwa na hukmu ya ki-Sheria.

Mchunguzi katika vitendo hivi ambavyo vimedokezwa na hukmu za ki-Sheria yanayo ambatana na twarika hupata kuwa vitendo hivyo ni vya ki-mada vinavyohakikisha natija ya kushikika na sio vitendo vinavyo hakikisha natija isioshikika hata kama aina hizi mbili za vitendo huhakikisha thamani moja. Mfano dua ni kitendo kinacho hakikisha thamani ya ki-roho na jihadi ni kitendo cha ki-mada kinacho hakikisha thamani ya ki-roho, lakini dua hata kama ni kitendo cha ki-mada lakini huhakikisha natija isioshikika nayo ni thawabu hata kama kusudio la mwenye kuomba dua ni kuhakikisha thamani ya ki-roho. Kinyume na jihadi ambayo ni kupigana na maadui nacho ni kitendo cha ki-mada kinacho hakikisha natija ya kushikika nayo ni kukomboa ngome au mji au kumuua adui na

yanayofanana na hayo, hata kama makusudio ya mujahid ni kuhakikisha thamani ya kiroho. Na kufikia hapa huwa vitendo vya ki-twarika ni vitendo vya ki-mada vinavyohakikisha natija ya kushikika na hukhtalifiana na vitendo venginevyo. Kwa hivyo haichukuliwi dua kama twarika ya jihadi hata kama mujahid humuomba Allah, kama haichukuliwi mawaidha kama twarika ya kumzuia mwizi hata kama hupewa mawaidha na huelekezwa (huongozwa). Asema ta'ala:

{ وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لاَ تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ لِلَّهِ } (البقرة: 193

"*Piganeni nawo mpaka hakuna tena fitna na dini yote iwe kwa Allah*" [TMQ 2:193] na asema ta'ala:

{ وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا} (المائدة: 38

"*Mwivi mwanamume na mwivi mwanamke, wakateni mikono yao*"[TMQ 5:38].

Kwa hivyo hukemewa kwa kila makemeo (msemo kwamba) vitendo vyote vinavyo kusudiwa kutekeleza fikra ya Uislamu ni vitendo visivyo hakikisha natija ya kushikika na huhisabiwa hilo kuwa ni kinyume na twarika ya Kiislamu. Na wala hakuna tofauti baina ya vitendo ambavyo hutumiwa kutekeleza hukmu zinazo ambatana na utatuzi wa matatizo na baina ya vitendo ambavyo hutumiwa kubeba da'wa ya Kiislamu. Mfano swala huchukuliwa ni katika fikra na twarika ya kuitekeleza ni serikali basi haijuzu serikali kuchukua mafundisho na mwongozo tu kuwa ni njia ya watu kusimamisha swala bali ni wajibu kuadhibu mwenya kuacha swala adhabu ya ki-mada kama kwa mfano jela na hata kama itasimama kufundisha na kuongoza. Na mfano wa hilo pia ni ubebaji wa da'wa ya Kiislamu ambayo ni fikra, na twarika ya kuitekeleza kupitia serikali ni jihadi yaani kupigana vita na maadui basi haijuzu kutumiwa masomo ya Sahihi ya Al-Bukhari kuondosha vizuizi vya ki-mada vilivyo mbele yake bali hapana budi kutumia jihadi nayo ni kupigana na maadui mapigano ya ki-mada. Na hivyo hivyo vitendo vyote.

Isipokuwa ni lazima ijulikane kuwa hata kama kitendo ambacho hudokezewa na twarika ni kitendo cha ki-mada kilicho na natija ya kushikika lakini hapana budi kupelekwa ketendo hichi kwa

maamrisho ya Allah na makatazo Yake na ikusudiwe katika kupelekwa kwake kwa maamrisho ya Allah na makatazo Yake kunali radhi za Allah. Kama pia hapana budi imtawale Mwislamu kudiriki kwake kwa fungamano lake na Allah ta'ala basi atajikurubisha kwake kwa swala, dua, kusoma Qur'an na mfano wake, na ni lazima aitakidi Mwislamu kuwa nusra (ushindi) hutoka kwa Allah. Kwa hivyo hapana budi iweko taqwa (uchaji-mungu) iliokita katika vifua ili kutabikisha hukmu za Allah. Na hapana budi kwa dua na hapana budi kudumu fungamano na Alla pindi zinapotendwa vitendo vyote.

Huu ni katika upande wa twarika na kuwa kwake hukmu za ki-Sheria ambazo ni wajibu tujilazimishe nazo wala tusizikhalifu, na katika upande wa vitendo na kuwa kwao vitendo vinavyo hakikisha natija ya kushikika. Amma kwa upande wa kufikia natija ni lazima ifuatwe qaida ya ki-vitendo, nayo ni kuwa kitendo hujengwa juu ya fikra na huwa kwa ajili ya lengo maalumu. Na hivyo ni kuwa hisia kwa tukio (*waqi'ah*) pamoja na elimu iliyotangulia ni lazima izae fikra na ni lazima iungane fikra hii na kitendo na iwe fikra na kitendo kwa ajili ya lengo maalumu, na yote hayo yabuniwe juu ya imani mpaka abakie mwanadamu katika mwenendo ndani ya mazingara ya ki-imani mwenendo wa daima. Wala haijuzu kata kata kutenganisha kitendo na fikra au na lengo maalumu au na imani; katika utengamano huu, jinsi utakavyo kuwa kidogo, ni hatari kwa kitendo chenyewe, kwa natija yake na kwa kudumu kwake. Kwa hivyo hapana budi lengo maalumu liwe ni lengo la kufahamika iliowazi kwa kila mwenye kutaka kutenda kitendo ili aanze nacho. Na ni lazima iwe mantiki ya hisia ndio msingi, yaani iwe fahamu na kufikiria ni zenye kutokamana na hisia wala situ kuwa mujarad ya mawazo juu ya qadhiya za ki-ndoto, na iwe hisia kwa *waqi'ah* ndio inayoathiri ubongo na pamoja na kuwepo elimu iliyotangulia kuleta harakati za kibongo ambazo ndio fikra. Na hii ndio inayohakikisha undani katika kufikiria na natija yake katika kitendo. Na mantiki ya hisia hupeleka kwa hisia ya kifikra yaani kwa hisia ambayo hutilia nguvu fikra kwa

mwanadamu. Kwa haya huwa kwa mfano hisia ya wabebaji da'wa baada ameifahamu ina nguvu kuliko hisia kabla hapo.

Na miongoni mwa hatari ni katika kugura kutoka hisia mpaka kitendo kichwa kichwa na sio kupitia fikra. Kwa sababu hii haibadilishi hali ilivyo (*waqi'ah*) bali humfanya mwanadamu ni mwenye kufuata mambo yalivyo na kuyaitikia: humpeleka ufahamu ulio didimia/zorota na hufanya hali ilivyo chimbuko la fikra sio mahala pa kufikiriwa. Basi hapana budi kwa hisia kufika mwanzo kwa fikra kisha ipelekwe fikra hii kwa kitendo. Na hii ndio huwezesha kunyanguka (kupanda juu) kutoka hali ilivyo na huwezesha kitendo kugura kuelekea hali nzuri kwa kugura ki-mapindizi. Yule anayehisi hali ilivyo kisha akatenda hatendi kubadilisha hali ilivyo bali hutenda ili kuiweka nafsi yake kwa mujibu wa hali ilivyo na hubakia nyuma na mwenye kuzorota. Na yule ambaye huhisi hali ilivyo kisha akafikiria jinsi ya kuibadilisha kisha akatenda kwa mujibu ya fikra hii, huyu ndiye anayebadilisha hali ilivyo kwa mujibu wa mfumo wake na hubadilisha mabadiliko ya ki-jumla. Huyu ndiye anayewafikiana na twarika ya ki-mapinduzi ambayo ndio twarika ya ki-pekee ya kuregesha maisha ya Kiislamu, kwa sababu njia hino hulazimisha kuwa fikra iwe ni natija ya hisia na iwe wazi fikra hii kiasi ambacho itachora ramani ya ki-ufundi kwa fikra na twarika katika akili. Basi mwanadamu hudiriki mfumo kudiriki kulio sahihi utakaompeleka kwa kutenda mpaka iwe fikra imezalisha ndani yake mapinduzi ya ki-jumla. Basi huendelea mbele wakati huo katika kuandaa watu, mujtama na mazingira kwa fikra hii ili izalishe mapinduzi katika rai jumla (*rai' 'amm*) baada ya kupatikana busara ya ufahamu jumla (*wai' amm*) juu yake mfumo kwa fikra na twarika. Kisha huanza katika njia ya kuhukumu katika kutabikisha mfumo utabikishaji wa ki-mapinduzi bila kukubali kutabikisha kidogo kidogo (*tadarruj*) au kupiga viraka. Na njia hii ya ki-mapinduzi hulazimisha fikra iwe ni natija ya hisia na iunganishwe na kitendo kwa ajili ya lengo maalumu, wala hakuna itakayo fikia hapa ila fikra ya ki-ndani.

Na fikra hii ya ki-ndani yahitaji mwenye kuileta au kuikuza na kufanya kama ardhi rutuba (*khasaba*). Na njia ya ki-mapinduzi huhitaji kuwaandaa watu kwa mfumo wa Kiislamu na kuandaa mujtama nao. Na kuileta fikra hiyo ya ki-ndani na kuandaa watu na mfumo hulazimisha kuusoma Uislamu kutoka wale ambao wataka kutenda na hulazimisha hivyo hivyo kuusoma mujtama, na hayapatikani hayo ila kwa njia ya kuukuza akili kwa maalumuti. Masomo ni njia ya sahali na ya karibu ya kufikisha maalumuti hizi kwa akili ili isaidie katika kuleta fikra.

Uislamu una njia makhsusi katika kufundisha na kuifuatilia ndio inayoleta athari kwa masomo haya. Njia hiyo ni kulazimisha kusoma maalumuti ili kutenda nayo na kupokea mafundisho hayo upokeaji wa ki-fikra unao athiri: huathiri katika hisia mpaka iwe hisia yake juu ya uhai na majukumu yake ni hisia ambayo ni natija ya ni fikra inayo athiri, mpaka ipatikane katika nafsi ya mwenye kusoma moto, hamasa, fikra na maarifa mengi kwa wakati mmoja na huwa utabikishaji ni natija ya ki-kawaida. Na njia hiyo katika mafundisho, juu ya kuleta ufahamu kwa mwenye kusoma na kuleta ndani yake uweza wa kutekeleza aliyoyafahamu kwa sura ya kuathiri, hakika yake hupanua fikra na huunganisha fikra na hisia na humfundisha mwenye kusoma uhakika ambao hutumiwa kutatua matatizo maishani. Kwa haya ni lazima iepukane mafunzo kuwa tu ni mujarad ya elimu tu, mpaka asiwe mwenye kusoma kuwa ni kitabu chenye kutembea na ili yasiwe ni mujarad ya mawaidha na miongozo ama itakuwa (*sathiya*) pasina joto la imani. Na ni lazima isichukuliwe mafundisho ya Kiislamu kuwa ni mafunzo ya mujarad ya ki-elimu na mawaidha bali huchukuliwa kuwa kwake ya elimu na mawaadha kuwa ni hatari kwa kitendo na kiepusha na kilevya kwake (kitendo).

Na kufikia lengo ambalo kwa ajili yake hutendwa, ni lazima ifahamike kuwa lengo hili ili kulifikia huhitaji kujitolea na kuipa umuhimu, na kujifunga na majukumu yaliyolazimishwa na jukumu la ki-chama juu ya majukumu ya Uislamu. Na Uislamu ina majukumu: (yenye) kukanya (*salibiyya*) na yenye kuamrisha

(*ijabiyya*). Na hayo ni yenye kukalifisha ki-mali na ki-wiliwili na ki-nafsi. Na miongoni mwake ni taklifu za faradhi na wajibu kwa kila mmoja, na miongoni mwake ni yale yaliyo juu ya faradhi na wajibu anayoyatenda kwa khiyari wale walio na mustawa wa juu wa ki-roho na wa ki-akili, nawo ni wale ambao wanataka kuzidi kujikurubisha kwa Allah ta'ala. Na kutenda kwa haya majukumu hapana budi ili kufikia kwa lengo. Kwa hivyo ni lazima kumakinisha nafsi na kuilazimisha kutenda majukumu katika faradhi kwa kila upande: ki-mali, ki-wiliwili na ki-nafsi mpaka ipatikane matarajio ya kufikia lengo.

Ili kitendo kuzaa natija, hapana budi kupeleleza mahali ambapo kitendo hicho huanzia na kikundi ambacho huanza kutendea nacho. Ndio, Uislamu ni wa ki-ulimwengu nao huwatazama wanadamu wote na huwachukulia wanadamu wote kuwa ni sawa wala hauupi uzito wowote ikhtilaf ya ki-mazingara, mahala, mchanga na yanayofanana na hayo katika ulinganizi bali huwachukulia wanadamu wote kuwa wanafaa kupokea ulinganizi na huwachukulia Waislamu ndio wanaohusika na kubalighisha ulinganizi huu kwa wanadamu wote. Lakini pamoja na hayo hauanzi na ulimwengu kwa sababu kuanza nayo huchukuliwa ni kitendo kinachofifia wala hakifikishi kata kata kwa natija yeyote bali hapana budi kuwa ianze kwa mtu binafsi na iwe mwisho iwe ni kwa ulimwengu. Kwa hivyo ni wajibu kubebwa ulinganizi katika mahali ambapo itakamilika ndani yake mpaka iwe ni nukta ya kianzio kisha huchukuliwa hapa au pengineo katika mahali ambapo itamakinika ndani yake ulinganizi kuchukuliwa ni nukta ya kugura inayogura kutokamana nayo ulinganizi katika njia yake kisha huchukuliwa hapo au kwengineko kuwa ni nukta ya kumakinika inayosimama ndani yake ulinganizi na kupelekwa katika njia yake ki-maumbile: Njia ya jihadi. Lakini hata kama mahali huchukuliwa kama mahala pa kitendo katika kila nukta, isipokuwa kile ambacho hugura kutoka nukta moja mpaka nukta nyengine ni ulinganizi sio mahali na hugura ulinganizi katika mahala pote ambapo hutendwa ndani yake katika wakati mmoja. Na hakika yake, hata kama ni lazima kulengwa mahali ambapo patakuwa

ni nukta ya kianzio kisha kuwepo nukta ya kugura na nukta ya kumakinika, isipokuwa kulengwa mahali katika kila nukta miongoni mwa nukta hizi tatu sio katika mzunguko ambao mwanadamu hutawala juu yake kwa sababu yeye haumiliki wala hawezi kuumiliki bali huingia katika mzunguko unaomtawala mwanadamu. Wala si juu ya mwanadamu ila kujipeleka kutenda vitendo ambavyo huingia ndani ya mzunguko anayotawala juu yake; amma vitendo ambavyo ni katika mzunguko mwengine hutukia kwa mujibu ya matakwa ya Allah na *qadha* Yake.

Amma kuchaguliwa nukta ya kianzio huwa kata kata katika mahali ambapo hupatikana ndani yake yule inayonawiri katika fahamu yake mwanga wa mwanzo wa ulinganizi na Allah humtayarisha kwa kubeba ulinganizi huo; waweza kuhisi watu tofauti tofauti kwa hisia hiyo lakini yule ambaye Allah amemtayarisha kubeba ulinganizi hajulikani mpaka atakapotokea na uanze ulinganizi katika mahala ambapo yeye huishi ndani yake. Na huwa mahala hapo ni nukta ya kianzio.

Amma nukta ya kugura, hakika yake hukoma kwa matayarisho ya mujtama kwa sababu mujtama hutofautiana katika fikra, hisia na nidhamu. Basi mahala ambapo huwa mujtama wake ni mzuri na mazingara mazuri huwa ni nukta ya kugura. Na aghlabu sana sana huwa mahali ambapo ni nukta ya kianzio huwa ndio nukta ya kugura hata kama hilo sio dharura kwa sababu mahala panaposuluhu kugura ni mahala ambapo hukithiri ndani yake dhulma za ki-siasa na za ki-uchumi na huvuka mipaka kumkanusha Allah na ufisadi.

Amma nukta ya kumakinika, hakika yake hukoma hivyo hivyo juu ya kufaulu ulinganizi katika mujtama basi mahali ambapo hauathiri ulinganizi katika mujtama wake haiwezi kujiweka kwa nafsi yake mazingara na haisuluhii kuwa ni nukta ya kumakinika jinsi watakavyo kuwa wengi idadi ya wabebaji mfumo. Na mahali ambapo humezwa ndani yake fikra na twarika kutoka kwa mujtama na kuenea mazingara husuluhu

kuwa ni nukta ya kumakinika vyo vyote itakavyo kuwa idadi ya wabebaji mfumo.
Kwa hivyo haijuzu kwa wabebaji ulinganizi kupima ulinganizi kwa idadi ya wabebaji wake. Kipimo hicho ni cha makosa wazi wazi na ni hatari kwa ulinganizi kwa sababu hubadilisha ubebaji ulinganizi kutoka mujtama mpaka kwa watu na hli husababisha kuchelewa na pia huenda likasababisha kuzorota katika mahali hapo. Na siri ya hilo ni kuwa mujtama haukubuniwa juu ya watu tu kama wanavyo waza wengi bali wati ni sehemu katika kundi, na kinacho unganisha baina ya watu hawo katika mujtama na sehemu nyengine ni fikra, hisia na nidhamu. Kwa hivyo hutumiwa ulinganizi kusahihisha fikra, hisia na nidhamu, na ulinganizi huu wa kikundi ni ulinganizi kwa mujtama sio watu binafsi. Na kusuluhishwa watu binafsi haiwi ila wawe viungu katika kikundi ya ki-jumuiya kinachobeba ulinganizi kwa mujtama. Kwa hivyo wabebaji ulinganizi wanaofahamu uhakika wake hutegemea juu ya mujtama kubeba ulinganizi kwake, na huchukulia kuwa kutengenea mtu binafsi haimkiniki kutengeneza mujtama bali haimkiniki kutengenea yeye kutengenea kulio kwa daima. Bali huwa kutengenea mtu binafsi kwa kutengenea mujtama, na pindi inapotengenea mujtama hutengenea mtu binafsi. Kwa hivyo ni wajibu ielekezwe ulinganizi wao kwa mijtama, na kuwa qaida ni: (Tengeneza mujtama atatengenea mtu binafsi na ataendelea kutengenea).

Kwa kuwa mujtama hushabihiyana na maji katika chungu kubwa, pindi inapowekwa chini yaku au pambizoni mwake kile kinachosababisha ubaridi hubaridika maji na hugeuka kuwa barafu. Hivyo hivyo inapowekwa katika mujtama msingi fisadi huwa katika ufisadi na hubakia katika kuzorota na kufifia, na pindi inapowekwa ndai yake msingi yanayo gongana hudhihirika katika mujtama mgongano na hubakia mujtama ukikorogeka katika mgongano na (*muyu'iya*) wake. Na pindi inapowekwa chini ya chungu moto inayochemsha na kuwasha moto, maji hushika moto kisha hutokota na huwa mvuke unaosukuma unaharikisha. Hivyo hivyo ikiwekwa katika mujtama mfumo sahihi huwa ni mwasho katika mujtama

inayobadilika kwa moto wake mpaka kutokota kisha huwa ni harakati na msukumo, na hutabikishwa mfumo na kubebwa ulinganizi wake kwa mijtama nyengine. Na hakika hata kama kubadilika mujtama kutoka hali moja hadi nyengine inayogongana au, kwa matamshi mengine, kupinduka kwake kutoka hali moja hadi nyengine haishuhudiwi kama isivyo shuhudiwa kubadilika maji katika chungu, lakini wajuzi wa mujtama wanaoamini kuwa mfumo wanaoubeba ni moto na nuru unaochoma na kuangaza hujua kuwa ni katika hali ya kubadilika na kuwa itafikia katika daraja ya kuchemka kisha kata kata itafikia katika daraja ya haraka na msukumo kwa hivyo hutia hamu kwa mujtama.

Kwa hayo, hakika mahali ambapo husuluhia kuwa ni pa kumakinisha hatuujui kwa sababu hukoma kwa kuandaliwa mujtama si tu juu ya nguvu ya ulinganizi. Hakika wa ulinganizi wa Kiislamu Makka ulikuwa na nguvu na pamoja na hilo Makka hata kama ilikuwa ni nukta ya kianzio chake na kusuluhia kuwa ni nukta ya kugura na ikagura kutoka kwake ulinganizi, lakini haikusuluhia kuwa ni nukta ya kumakinika bali ilikuwa nukta ya kumakinika katika Madina. Kwa hivyo aliguria Mtume (SAAW) baada ya roho yake kutua na mutjama wake, na akasimamisha Madina ambao kutokamana nayo iligura ulinganizi kwa nguvu kwa mabakio ya pembe za bara Arabu na kisha kwa dunia yote.
Na kufikia hapa, twaweza kusema kuwa wabebaji ulinganizi haimkiniki kwao wao kujua mahali ambapo husuluhia kuwa nukta ya kugura wala mahali ambapo husuluhia kuwa nukta ya kumakinika, wala haimkini kwao wao kujua vyovyote watakavyo kuwa mahadori na udadisi bali elimu ya hilo iko kwa Allah ta’ala. Kwa hivyo ni wajibu kuwa mategemeo ya wabebaji ulinganizi yawe kwa kitu kimoja nayo ni imani kwa Allah ta’ala na iwe vitendo vyao vyote visimame tu juu ya imani hii sio juu ya chengine. Na kwa imani juu ya Allah sio kwa mwengine hufaulu ulinganizi.

Na imani kwa Allah hulazimisha ukweli wa kumtegemea Yeye, na kutaka msaada kutoka Kwake kwa sababu Yeye peke Yake

ndiye anayejua siri na yaliyofitamana, na Yeye ndiye anayewapa taufiq wabebaji ulinganizi na kuwaongoza njia ya sawa na njia ya uongofu. Kwa hivyo hapana budi na nguvu ya imani na hapana budi na ukamilifu wa kumtegemea Allah, na kudumu kutaka msaada kutoka Kwake ta’ala. Na imani humlazimisha muumini kuamini mfumo yaani imani kwa Uislamu kwa sababu hutoka kwa Allah ta’ala na hulazimu iwe imani iliyokita iliyothibiti isiyokuwa na shaka wala hakuna uwezekano wa kupenya shaka kwa sababu kila hatari ya shaka katika mfumo hupelekea kwa uzorotefu bali huenda likapelekea katika ukafiri na uasi (twajilinda na Allah kwa hayo).

Imani hii iliyo na nguvu ambayo isiopenya kwake shaka ni jambo la lazima kwa wabebaji ulinganizi kwa sababu ndiyo inayodhamini kudumu mwenendo wa ulinganizi kwa njia ya haraka pana katika njia iliyonyoka. Na imani hii huwajibisha ulinganizi uwe wazi unayopambana na kila kitu; utapambana na ada na desturi, fikra za kigonjwa, ufahamu uliokorogeka, utapambana hata na rai amma ikiwa ni ya ki-makosa hata kama itazuiliwa katika kupambana nayo. Itapambana na itikadi na dini hata kama itakabiliana na balaa za wafuasi wake. Kwa hivyo hutofautika ulinganizi uliojengwa juu ya aqeeda ya Kiislamu kwa uwazi, shujaa na nguvu, na fikra na hupambana na kila anayekhalifu fikra na warika na kukabiliana naye ili kubainisha ubovu wake bila kujali natija yake na matokea yake, na bila kujali aghlabu ya Umma utawafikiana au wataukataa na kuupinga. Kwa hivyo mbebaji ulinganizi hawasifu kwa kuvuka mipaka watu wala kuwapaka mafuta, wala kuwanyenyekwa wale wanaomiliki uzito katika mujtama miongoni mwa viongozi na wengine wala hawaonyeshi urafiki bali hushikamana kwa mfumo pekee yake bila kuingia katika hisabu ya kitu chochote isiyokuwa mfumo.

Imani hii pia huwajibisha ubwana uwe kwa mfumo pekee yaani Uislamu pekee yake bila mwengineo na kuchukuliwa mwengineo katika mifumo kuwa ni ukafiri jinsi zitatakvyo tofautika na kukhtalifiana mifumo:

{ إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الإِسْلَامُ } (آل عمران: 19

"*Kwa hakika, dini mbele ya Allah ni Uislamu*" [TMQ 3:19].

Kila asiyeamini Uislamu ni kafiri katika mtazamo wa Kiislamu kwa hivyo haijuzu kata kata kwa mbebaji ulinganizi wa Kiislamu kuwaambia wanaobeba usiokuwa Uislamu sawa sawa ikiwa ni dini au mfumo: 'Shikamaneni na mfumo wenu na dini yenu' bali ni wajibu awalinganie kwa Uislamu kwa hika na mawaidha mema ili wasilimu kwa sababu ulinganizi hulazimu wabebaji wake wafanye kazi ili ubwana uwe kwa Uislamu peke. Na sio maana ya kuwawacha wasiokuwa Waislamu na dini yao na wanayo yaitakidi kuwa ni kukiri dini zao bali ni kuitikia amri ya Allah ambao amewajibisha kutolazimisha watu kuukubali Uislamu kwa nguvu na akawajibisha kuwawacha watu na itikadi zao, dini zao na ibadi zao maadamu itabakia ki-binafsi sio kijumla na wasiwe na umbo (*kiyan*) ndani ya utawala wa Uislamu. Kwa hivyo hukataza kuwepo vyama au makundi ya ki-siasa yasiyokuwa ya Kiislamu yanayosimama juu ya msingi unaogongana na Uislamu, na huruhusu vyama na makundi yaliyo ndani ya Uislamu. Hivi ndivyo inavyoamrisha imani kwa mfumo kwa watu wake pekee yake kwa mujtama wala wasishirikiane pamoja nao yeyote asiyekuwa wao.

Na imani kwa Uislamu ni tofauti na kufahamu hukmu na Sheria zake kwa sababu imani juu yake imethubutu kwa njia ya akili kwa hivyo haipenyi ndani yake shaka. Amma kufahamu hukmu zake, hilo halikomi kwa akili peke yake bali hukoma juu ya kujua lugha ya kiarabu, nguvu ya *istinbat* na kuzijua hadithi sahihi kutoka hadithi dhaifu. Kwa hivyo imekuwa juu ya wabebaji ulinganizi kuchukua fahamu za wengineo kuwa ni za ki-makosa zilizo na uwezekano wa kupata mpaka iwezekane kwao kuulingania Uislamu na ahkamu zake kwa mujibu ya fahamu zao kwake na *istinbat* zao kwake, na waweze kubadilisha fahamu za wengineo ambazo wanazichukulia kuwa ni za ki-makosa zilizo na uwezekano wa kupata kwa fahamu zao wanazozichukulia kuwa ni za sawa zilizo na uwezekano kukosa. Kwa hivyo haisihi kwa wabebaji ulinganizi kusema juu ya

ufahamu wao kuwa ‘hino ni rai ya Uislamu’ bali ni juu yao kusema juu ya rai yao kuwa ‘hino ni rai ya Kiislamu.’ Walikuwa watu wa madhabu miongoni mwa mujtahidina wakichukulia *istinbat* zao kwa ahkamu kuwa ni sawa inayobeba uwezekano wa kukosa, na kila mmoja wao walikuwa wakisema ‘inaposihi hadithi basi hio ndio madhab yangu na ipigeni kauli yangu kwa kikuta.’ Hivyo hivyo ni wajibu wabebaji ulinganizi kuchukulia rai zao ambazo wamezi-tabanni au kuzifikia kutoka Uislamu kwa kuchukua fahamu zao ni rai za ki-sawa zinazobeba uwezekano wa kukosa katika wakati ambao imani yao kwa Uislamu ni aqeeda isiojuzu kupenya ndani yake shaka yeyote. Bali huchukua wabebaji ulinganizi fahamu zao kwa kuchukua hiko kwa sababu ulinganizi unapanda katika nafsi zao hamu ya kutaka ukamilifu, na huwalazimisha daima kuchunguza uhakika na daima kuchunguza kila wanalolijua na kulifahamu mpaka waisafishe kutoka kila kigeni ambacho huenda kime gandamana nacho, na kuweka mbali kila kinacho jikurubisha nacho kwa uwezekano wa kujiunga nayo na kuchukuliwa kuwa ni sehemu yake; na hilo mpaka fahamu ibakie ni sahihi na fikra ya kindani, na mpaka ibakie fikra ni nyeupe na safi kwa sababu kwa kadri ya usafi wa fikra ya uweupe wake huwawezesha kusimamia ulinganizi. Kwa sababu usafi wa fikra na uwazi wa twarika ndio dhamana ya kipekee ya kufaulu na kuendeleza ufaulu.

Isipokuwa uchunguzi (*tanqib*) huu juu ya uhakika wa kutafuta la usawa haimaanishi kuwa fahamu zao zimepeperuka na upepo bali ni lazima fikra ya kindani, kwa hivyo huwa ni fahamu iliyo thubutu kuliko fahamu yeyote isiokuwa hivyo. Kwa hivyo imekuwa juu ya wabebaji ulinganize kwa macho kuwa ulinganizi wao ni katika ufahamu wao kwanzo, wakitahadhari kufitiniwa na wengineo kwa ulinganizi wao, na fitna hii ni hatar iliyo mbaya kwa ulinganizi, kwa hiyo Allah alimhadharisha nayo Mtume wake (SAAW):

**{ وَاحْذَرْهُمْ أَنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنزَلَ اللَّهُ إِلَيْكَ } (المائدة: 49**

“*Nawe jihadhari nawo wasikufitinishe na baadhi ya yale aliyokuteremshia Allah*” [TMQ 5:49].

Na akasema Bwana Umar kwa kadhi wake Shuraih pindi alipokuwa akimuusia kutizama katika Kitabu cha Allah, akamwambia “watu wasikupotoshe kutokamana nayo.” Kwa hivyo ni lazima watahadhari wabebaji ulinganizi kutoka tamko ambacho kwenda kitaotoka kutoka mwenye ikhlasi au rai huenda akaiona mwenye pupa kwa ulinganizi na kuiandamisha kwa hoja ya maslahi na ilhali inakhalifu Uislamu, basi atahadhari nayo wala asikubali hilo kutokamana na yeyote, kwa sababu katika hayo kuna upotevu uliowazi, na ni lazima ulinganize kwa kurudisha Uislamu maishani na pia ni lazima kutofautisha baina ulinganizi kwa Uislamu na ulinganize kwa kurudisha Uislamu maishani na pia ni lazima kutofautisha baina ulinganizi na kundi katika Ummah kama kikundi cha Uislamu na baina ya ulinganizi unaobebwa na serikali ya Kiislamu.

Amma kutofautisha baina ya ulinganizi kwa Uislamu na ulinganizi wa kurudisha Uislamu maishani, huwa ili kujua lengo ambalo ulinganizi inajipeleka kwayo. Na tofauti baina yake ni kuwa hubebwa ulinganizi kwa Uislamu kwa wasiokuwa Waislamu na hulinganiwa ili waukubali na kuingia ndani yake na hawa huwa njia ya kivitendo ya kuwalingania ni kuhukumiwa na Uislamu kupitia serikali ya Kiislamu mpaka waone nuru ya Uislamu; na hulinganiwa kwa Uislamu katika kubainisha aqeeda yake na hukmu zake mpaka wadiriki ukubwa wa Uislamu. Kwa hivyo imekuwa ni lazima serikali ya Kiislamu kubeba ulinganizi kwa Uislamu.

Amma ulinganizi wa kurudisha maisha ya Kiislamu ni lazima ubebwe na kikundi wala si na watu binafsi. Na ulinganizi huu wa kurudisha maisha ya Kiislamu ni: Kuna mujtama ambao huwa watu wake kwa jumla yao ni Waislamu na huhukumiwa na yasiyokuwa Uislamu, huwa ni mujtama usiokuwa wa Kiislamu na husimama juu yake kuwa ni Dar al-Kufr. Na hulinganiwa ndani yake ili isimame serikali ya Kiislamu itakayo tabikisha Uislamu ndani yake na kubeba ulinganizi wake kwa wengineo. Hili ikiwa hakuna serikali ya Kiislamu kata kata; na ikiwa kuna serikali ya Kiislamu inyotabikisha Uislamu

kikamilifu hulinganiwa ndani yake ili iwe eneo katika eneo la serikali ya Kiislamu ili ihukumu kwa upande wake na Uislamu na ili iwe ni sehemu yake. Hubebwa ulinganizi wa Kiislamu mpaka iwa mujtama wa Kiislamu ni itakuwa kweli wakati huo kuwa ni Dar al-Islam. Kwa sababu haijuzu kwa Mwislamu kuishi katika Dar-ul-Kufr bali ni juu yake pindi inapokuwepo Dar al-Islam na ilhali yeye ywaishi katika Dar-ul-Kufr kufanya kazi ili aifanye kuwa ni Dar-al-Islam au agurie Dar al-Islam.

Amma kutofautisha baina ulinganizi unaobebwa na kikundi katika Ummah wa Kiislamu na baina ya ulinganizi unaobebwa na serikali ya Kiislamu, hino ni kujua aina ya kazi ambao hufanya wabebaji ulinganizi. Na tofauti baina yake ni kuwa ulinganizi unaobebwa na serikali ya Kiislamu humathilika ndani yake upande wa kivitendo nao ni kutabikishwa Uislamu kwa ndani utabikishaji kamilifu na kijumla mpaka Waislamu wanali kufaulu (*sa'ada*) maishani na aone asiokuwa Mwislamu wanaoishi ndani ya utawala wa serikali ya Kiislamu nuru ya Uislamu, basi wataingia wenyewe kwa khiyari zao wakiwa na radhi na utulivu. Na itabeba (yaani serikali) ulinganizi wa kiinje, si tu kwa njia ya matangazo na kusherehesha hukmu za Kiislamu bali kwa kuandaa nguvu kwa jihadi katika njia ya Allah, kwa ajili ya kuhukumu biladi ambazo ni jirani ya Uislamu, ikichukulia kuwa kuzihukumu na Uislamu ndio njia ambayo aloitumia Mtume (SAAW) na pia ilitumiwa na ma-Khalifa wake baada yake mpaka serikali ya mwisho ya Kiislamu. Kwa hivyo imekuwa kubebwa ulinganizi na serikali ndio upande wa kivitendo katika ulinganizi wa kindani na ki-nje.

Amma ulinganizi ambao hubebwa na kundi au kikundi, hizo ni vitendo vinavyo ambatana na fikra wala haziambatani na kutenda vitendo venginevyo. Kwa hivyo huchukuliwa upande wa ki-fikra sio upande wa kivitendo. Itasimama kwa kitendo yaliyo faradhishwa juu yake na Sheria katika mfano wa hali hino, mpaka ipatikane serikali ya Kiislamu kisha ianze upande wa kivitendo katika serikali. Na hayo ni pamoja na kuwa

huwalingania Waislamu, lakini huwalingania kuufahamu Uislamu mpaka warudishe maisha ya Kiislam, na kupambana na kila anosimama mbali ya ulinganizi huu kwa mbinu ambayo inayowajibisha mapambano nawo.

Na ni lazima yachukuliwe maisha ya Mtume (SAAW) akiwa Makkah kuwa kiigizo ya kufuata kwa mujibu wake katika ulinganizi. Itaanza katika hatua ya kusoma na kufahamu pamoja na kutenda yanayo lazimishwa na Uislamu kama ilivyokuwa hali katika nyumba ya Arqam, kisha watagura wanaosoma waliofahamu Uislamu, waumini wakweli kwa kuingiliana na Ummah mpaka waufahamu Uislamu na wafahamu dharura ya kuwepo serikali ya Kiislamu. Na ni juu ya kundi kuanzia watu kwa kutaja ufisadi wao na kuiaibisha, na kupambana na fahamu zao zilio changanyikiwa na rai zao zilizofisidika na kuzisafihi. Na kuwabainisha uhakika wa Uislamu na kiini cha ulinganizi wake mpaka iwapo kwao wote ufahamu wa busara jumla (*wai' 'amma*) juu ya ulinganizi. Na kuwa watu wa ulinganizi ni sehemu ya Umma, na utakuwa Umma pamoja nao kwa jumla bila kugawanyika, na utafanya kazi Umma kwa ujumla wake kazi iliyo na natija chini ya uongozi wa kundi la ulinganizi, mpaka wafikie katika utawala na waiunde serikali ya Kiislamu. Na wakati huo utachukuliwa maisha ya Mtume (SAAW) akiwa Madina kama kiigizo cha kufuata kwa mujibu wake katika kuutabikisha Uislamu na kubeba ulinganizi kwake. Na kwa haya kundi la Kiislamu ambalo hubeba ulinganizi kwa halino mahusiano na upande wa kivitendo, wala haijishughulishi na kitu chochote kisichokuwa ulinganizi. Na huchukulia kutenda kitendo chochote miongoni mwa vitendo vinginevyo kuwa vya kupumbaza, kupotosha na kikwazo kwa ulinganizi, wala haijuzu kata kata kujishughulisha nazo. Mtume (SAAW) alikuwa akiulingania Uislamu Makka ilhali Makka umejaa ufasiki na uovu wala hakutenda kitendo chochote cha kuziondoa na ilikuweko dhulma, unyanyasaji na ufukara wala haikupokelewa kutokamana naye kama ametenda kitendo ili kukhafifisha vitu hivyo. Na ilikuwa katika ka'aba na masanamu yanayopita kimo chake na wala haikupokelewa kutokamana naye kama aligusa

sanamu yeyote katika yale. Bali alikuwa akiyaaibisha miungu yao na kuzisafihi ndoto zao na kuzitia ubayani vitendo vyao, na alifunguka na kusema tu na kwa upande wa ki-fikra. Lakini pindi alipokuwa na serikali na akaikomboa Makka hakubakisha chochote katika masanamu hayo, wala ufasiki na uovu huo, wala dhulma na unyanyasaji, wala ufukara na umasikini.

Na kwa hivyo haijuzu kwa kundi ikiwa inabeba ulinganizi kutenda kama kundi kitendo chochote miongoni mwa vitendo vyengineo, na ni lazima ibakie tu kwa fikra na ulinganizi isipokuwa watu hawazuiliwi kutenda wanayoyataka miongoni mwa vitendo vya msaada lakini kundi halitendi hayo kwa sababu kazi yake ni kusimamisha serikali na kubeba ulinganizi.

Pamoja na kuwa ni lazima kuchukuliwa maisha ya Mtume (SAAW) akiwa Makka kama kiigizo cha kukifuata kwa mujibu wake, yapasa kutambuliwa tofauti baina ya watu wa Makka na kulinganiwa kwao kwa Uislamu na baina ya Waislamu leo na kulinganiwa kwao kurudisha maisha ya Kiislamu. Nayo ni kuwa Mtume (SAAW) alikuwa akiwalingania makafiri kwa imani na amma ulinganizi leo ni kuwalingania Waislamu ili waufahamu na watende nao.

Kwa hayo imekuwa ni lazima kwa kundi isijichukulie nafsi yake kuwa tofauti na Ummah ambayo huishi pamoja nayo, bali kujichukulia nafsi yake kama sehemu ya Ummah huo kwa sababu watu ni Waislamu kama wao. Na wao sio bora kuliko yeyote miongoni mwa Waislamu hata kama wameufahamu Uislamu na kuutenda, isipokuwa wao wamebeba mzigo mkubwa kuliko Waislamu, na walishikilia na kufuata zaidi mas’uliya ya kuwatumika Waislamu mbele ya Allah na kufanyia kazi Uislamu. Na ni juu ya watu wa kundi la Kiislamu kujua kuwa hawana thamani jinsi watakavyo kuwa wengi idadi yao bila ya Ummah ambayo wanafanyia kazi ndani yake. Kwa hivyo imekuwa jukumu lao ni kuingiliana pamoja na Ummah na kutembea pamoja nao katika mapambano na kuwatia hisia kuwa Ummah ndio unaofanya kazi. Na ni lazima kwa kundi kujiweka

mbali na kila kitendo au kauli au ishara itakayo onyesha utengamano wake na Umma kwa kitu chochote kiwe kidogo au kikubwa kwa sababu hili huitenganisha Ummah na ulinganizi wake na kufanya fundo katika mafundo ya mujtama ambao hivo ni kikwazo unaozuia mwamko wake. Ummah ni jumla usiogawanyika, ikisimama kundi ili kusimamisha serikali na itabakia kuwa ni mlinzi wa Uislamu katika Ummah na serikali na ikiona katika Ummah mgeuko (kutoka haki) itaitanabahisha na imani yake na uhodari wake. Na itakapoona katika serikali ukombo itashirikiana pamoja na Ummah ili kuinyosha kwa yale yaliyofaradhishwa na Uislamu. Kwa hivyo huenda ulinganizi wa Kiislamu inayobebwa na kundi katika njia yake ya ki-kawaida ya kipekee.

Basi lengo la kundi ni kurudisha maisha ya Kiislamu katika biladi za Kiislamu na kubeba ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu, na njia yake ya kufikia hayo ni utawala. Na katika njia yake ya kufikia utawala ni kuusoma Uislamu na kuufahamu na kuwajenga watu kwa thaqafa itakayo leta athari katika kuleta akili ya Kiislamu na nafsiya ya Kiislamu ili kujenga shakhsiya ya Kiislamu, na hivyo hivyo kuingilana na Umma ili kuufahamisha Uislamu na kuufahamisha uhakika wa maslahi zake na suluhisho za Uislamu kwayo na kudhamini kuyahakikisha na ku-tabanni maslahi ya Umma. Na iendeshwe maingiliano na mapambano katika njia ya ulinganizi pamoja na mafundisho katika wakati mmoja. Kazi hii kutoka kundi cha ki-chama ni kazi ya kisiasa, kwa hivyo hapana budi uwe upande uliowazi wa kundi hili ni upande wa kisiasa kwa sababu ndio njia ya kivitendo ya mwanzo ambao huanza ndani yake ulinganizi kwa Uislamu. Na hii haimaanishi kuwa ni ulinganizi kwa siasa tu au kwa utawala tu, bali humaanisha ulinganizi kwa Uislamu na mapambano ya kisiasa ili kufikia kwa kutawala kamili, na ili kuleta serikali ya Kiislamu ambayo itatabikisha Uislamu na kubeba ulinganizi wake. Kwa hivyo huwa ni lazima kundi itakayobeba ulinganizi wa Kiislamu kuwa kundi la kisiasa wala haijuzu liwe ni kundi la kiroho, wala kundi la ki-akhlaqi, wala kundi la kielimu wala kundi la kuelimisha wala kitu

chochote kati ya hayo na yanayo shabihiyana nayo. Bali ni lazima iwe ni kundi la kisiasa, na kwa hapa imekuwa Hizb-ut-Tahrir ni chama cha Kiislamu–ni chama cha kisiasa inayojishughulisha na siasa na inayofanya kazi ili kuwajenga Ummah na thaqafa ya Kiislamu, na hudhihirika ndani yake upande wa kisiasa. Na huyakemea yanayofanywa na wakoloni na vibaraka wao kwa kuwazuia wanafunzi na wafanyi kazi na siasa na kujaribu kuwaweka watu jumla mbali nao, na huona kama ni lazima watu wajue siasa na idhihirike kwao malezi ya kisiasa. Sio katika kazi ya kisiasa kuwabainishia watu kuwa Uislamu hujumulisha siasa wala kuwa misingi ya kisiasa katika Uislamu ni hivi na hivi, bali siasa ni kuchunga maslahi ya Ummah mzima kindani na ki-nje na kuuendesha kwa mwenendo wa Kiislamu sio mwengine na yawe hayo kutokamana na serikali na kutokomana na Ummah ikihisabu serikali juu yake. Na mpaka yatokee hayo kivitendo hapana budi iwe chama ndicho kinachosimamia hayo katika Umma na katika utawala, na kwa hivyo hubeba ulinganizi wa Kiislamu ulinganizi jumla na kubainisha kwa Umma hukmu za ki-Sheria ambazo hutatua matatizo ya ki-maisha. Na hufanya kazi ili Uislamu uhukumu pekee na kupigana jihadi na mkafiri mkoloni kumng’oa kutoka mizizi yake sawa sawa wawe ndio wanaobeba fikra kiongozi na mfumo wake na wanaobeba siasa zake na fikra zake.

Na kubeba ulinganizi wa Kiislamu na mapambano ya kisiasa ni katika njia yake na huwa katika mujtama ambao chama kimekilenga kama majaal yake. Na Hizb ut-Tahrir huuchukua mujtama wa Kiislamu ulimwenguni kote ni mujtama mmoja kwa sababu suala lake lote ni suala moja nalo ni suala la Uislamu lakini imefanya nukta ya kianzio kuwa ni biladi ya kiarabu kwa sifa yake kama sehemu ya biladi ya Kiislamu, na huona kama kusimama kwa serikali ya Kiislamu katika biladi ya kiarabu kama kiini cha serikali ya Kiislamu ni hatua ya kawaida katika hayo.

Na mujtama katika ulimwengu wa Kiislamu uko katika ustawi mbaya wa kisiasa nao kwa jumla yake umefanywa ukoloni na serikali za kimagharibi, na umebakia katika ukoloni hata kama

Ummah unaona dhihirisho la utawala na kindani. Nao umenyenyekea kwa uongozi wa kifikra wa ki-rasilimali wa kidemokrasia unyenyekevu kamili, na kutabikishwa juu yake katika utawala na siasa kwa nidhamu ya kidemokrasia. Na katika uchumi kwa nidhamu ya kirasilimali, nao katika upande wa kijeshi inaoongozwa na wageni katika silaha zake, mazoezi yake na fani zilizo salia za kijeshi, na katika siasa ya kigeni inafuata siasa za kigeni za mwenye kuifanyia ukoloni. Kwa hivyo twaweza kusema kuwa biladi ya Kiislamu baado imebakia katika ukoloni na baado ukoloni umekita ndani yake, kwa sababu ukoloni ni kulazimisha utawala wa kijeshi, kisiasa, ki-uchumi, na ki-thaqafa juu ya watu dhaifu ili kuwanyonya, nayo hutumia nguvu zote ili kulazimisha uongozi wake wa ki-fikra na kumakinisha mtazamo wake maishani. Na sampuli za ubeparti tofauti tofauti unajumulisha kuunganishwa kwa nchi iliyoshindwa kwa ardhi ya nchi inayokoloni na kuanzisha koloni na kusimamishwa kwa serikali huru kijina lakini kivitendo inanyenyekea kwa serikali iliyoikoloni. Huu ndio hakika (waqi'ah) katika biladi za Kiislamu, uhakika wake ni kuwa zote zinanyenyekea kwa utawala wa ki-magharibi na hupelekwa kwa mujibu wa mpango wa kikoloni wa ki-magharibi katika upande wa ki-thiqafa. Na pamoja na kunyenyekea kwake kwa utawala wa ki-magharibi, zimekuwa hivyo hivyo ni lengo la uvamizi wa umoja wa kisovieti wa zamani pindi ilipokuwa ikifanya kazi ndani yake kwa kupitia vibaraka vyake ili watu wauamini ukomunisti, na ili itawale uongozi wake wa ki-fikra na mtazamo wake maishani kwa kulingania mfumo wa kikomunisti.

Kwa hayo, zimekuwa biladi za Kiislamu ni koloni za serikali ya ki-magharibi na uwanja kwa uongozi za ki-fikra za kigeni, na hivyo hivyo zilikuwa ni kituo cha macho ya umoja wa kisovieti wa zamani na lengo la uvamizi wake na kutekwa kwake si kwa ajili ya kuzikoloni bali kuzibadilisha biladi za Kiislamu kuwa biladi ya kikomunisti, na kuibadilisha mujtama wote iwe ni mujtama wa kikomunisti utakao futwa ndani yake athari ya Uislamu. Isipokuwa kwa kuanguka kwa umoja wa kisovieti yamepotea yote hayo hata kama wamebakia baadhi wanao

jinasibisha na vyama ya kikomunisti katika biladi za Kiislamu bila ya kuwa na uweza wowote wa kuathiri.

Na kufikia hapa imekuwa ni lazima kutekelezwa kazi ya kisiasa ili ipambane na ukoloni, na ipigane na uongozi za ki-fikra za kigeni na kufanya kazi ili kujikinga na hatari ya uvamizi wa kigeni ambayo inalenga biladi zetu. Kama ilivyo kubeba ulinganizi wa Kiislamu kubebwa kulio sahihi kupambana na hatari ya uongozi za ki-fikra za kigeni. Basi ni lazima iwe kupambana na ukoloni wa ki-magharibi ni jiwe la kiuno katika mapambano ya kisiasa.

Na mapambano ya kisiasa hulazimu kutopokea msaada ya kigeni kutoka mgeni wa aina yeyote na kwa upande wowote, na huhisabiwa kila msaada wa kisiasa kutoka kwa mgeni yeyote na kila kumlingania kwake yeye kuwa ni khiyana kwa Ummah. Na hulazimu pia kufanya kazi ili kujenga umbo (*kiyan*) la kindani katika ulimwengu wa Kiislamu mjengo mzuri ili liwe na nguvu ya ki-ulimwengu lilio na utawala wake wa kipekee, na mujtama wake uwe ni wa kutukuka. Na nguvu hii itafanya kazi ili ichukue nguvu za uongozi (*zimam al-mubadara*) kutoka kila mwanajeshi ili ibebe ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu na kutawalisha uongozi wake. Na pia hulazimu mapambano ya kisiasa kupigana vita na nidhamu, kanuni na sheria za ki-magharibi na hali zote za ukoloni kama pia ni lazima kukataa mipango yote ya ki-magharibi khasa khasa za Uingereza na Amerika, sawa sawa ziwe ni mipango ya kisanii au ya ki-mali kwa aina zake au mipango ya kisiasa kwa aina zake. Na hulazimu pia kupinga (*nabadha*) kata kata hadhara ya ki-magharibi, wala hilo haimaanishi kupinga aina tofauti za ki-madaniyya kwa sababu madaniyya huchukuliwa ikiwa ni natija ya elimu (sayansi) na usanii. Na hulazimu pia kung'oa uongozi wa ki-fikra wa kigeni kutoka mizizi yake. Na hivyo hivyo hulazimu pia kupinga thaqafa ya kigeni ambao hugongana na mtazamo za kifikra wa Kiislamu, wala hilo haimaanishi elimu (sayansi) kwa sababu elimu ni ya ki-ulimwengu na ni wajibu

kuchukuliwa kutoka upande wowote ule kwa sababu elimu ni katika sababu muhimu ya utangulizi wa ki-mada maishani.

Na mapambano ya kisiasa hulazimisha tujue kuwa wakoloni wa ki-magharibi khasa khasa Uingereza na Amerika hutegemea katika kila biladi koloni kusaidia vibaraka vyao katika watu walioregelea nyuma (*raji'iyin*) walio ndani ya giza, na wanaolingania kwa siasa zao na uongozi wao wa ki-fikra, na vikundi vinavotawala. Hukimbilia kuwapa msaada vibaraka hawa katika maeneo mbali mbali ili kuzuia harakati hino ya Kiislamu, na watawapa msaada wa ki-mali na usiokuwa wa ki-mali na kujumuisha nguvu zinazolazimu ili kuimaliza (harakati hino). Na utasimama ukoloni pamoja na vibaraka vyake kwa kubeba bendera ya uvumi dhidi ya harakati hino ya ukombozi ya Kiislamu kwa kuituhumu kwa tuhma mbali mbali: Kama kuwa wameajiriwa na wakoloni, huleta fitna ya kindani, ni yenye kupelekea ulimwengu kuwageukia Waislamu, inakhalifiana na Uislamu na tuhma nyenginezo zenye kufanana nazo. Kwa hivyo ni lazima wawe macho wenye kupambana juu ya siasa za kikoloni na mbinu zake mpaka wafichue njama zake za kikoloni za kindani na nje kwa wakati wake, kwa sababu kufichua njama za ukoloni kwa wakati wake huhisabiwa ni katika aina muhimu ya mapambano.

Na kwa hayo, hakika Hizb ut-Tahrir hufanya kazi ili kukomboa maeneo ya Kiislamu kutokamana na ukoloni wote, na hupigana vita na ukoloni vita visivyokuwa na mapumziko ndani yake. Lakini hailengi tu kuifukuza wala uhuru wa kirongo bali hufanya kazi ili kung'oa hali ambayo zimesimamishwa na kafiri mkoloni kutoka mizizi yake kwa kukomboa biladi, taasisi na fikra kutokamana na kutawaliwa (*ihtilal*) sawa sawa iwe kutawaliwa ki-askari au ki-fikra au ki-thiqafa au ki-uchumi au yasiokuwa hayo. Na hupigana vita na kila anayetetea upande wowote wa upande wa kikoloni mpaka yarudishwe maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha serikali ya Kiislamu ambayo itabeba ujume wa Uislamu kwa ulimwengu wote. Twamuomba Allah, na kwake Yeye twanyenyekea, atusaidie na msaada

kutoka Kwake ili tutekeleze majukumu haya mazito. Hakika Yeye husikia na ni mwenye kujibu.

## *HIZB- UT-TAHRIR.*

Hizb ut-Tahrir ni chama cha kisiasa na mfumo wake ni Uislamu. Lengo lake ni kurudisha maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha serikali ya Kiislamu itakayo tekeleza nidhamu za Kiislamu na kubeba ulinganizi wake kwa ulimwengu. Na imekwisha andaa Hizb hino thaqafa ya ki-chama iliodhamini hukmu za Kiislamu katika mambo ya ki-maisha. Na Hizb hulingania kwa Uislamu (kama) uongozi wa ki-fikra unaotokamana kwayo nidhamu ambazo hutatua matatizo yote ya mwanadamu, ya kisiasa, ya ki-uchumi, ya ki-thiqafa, ya ki-jamaa na mengineo yasiokuwa hayo. Nacho ni chama cha kisiasa inayo unganisha katika uwanachama wake wanawake kama inavyo unganisha wanaume. Na hulingania watu wote kwa Uislamu na ku-tabanni ufahamu wake na nidhamu zake, na huwatizama wote vyovyote watakavyo tofautika makabila yao na madhahibu zao kwa mtazamo wa Kiislamu. Na hutegemea kuingiliana na Ummah ili kufikia lengo lake, na hupambana na ukoloni kwa aina zake zote na majina yake yote ili kuhakikisha kukomboa Ummah kutokamana na uongozi wake wa ki-fikra na kung'oa mizizi yake ya ki-thiqafa, kisiasa, kijeshi na ki-uchumi na mengineo kutoka mchanga wa biladi za Kiislamu, na kubadilisha fahamu za makosa zilizo enezwa na mkoloni kufupisha Uislamu kuwa ni ibada na akhlaqi tu.